TAARIFA YA MAFANIKIO YA MIAKA 3 YA SERIKALI YA AWAMU YA 5 KATIKA WILAYA YA MONDULI KWA KIPINDI CHA MWAKA 2015 HADI 2018

1.0 Utangulizi:

Wilaya ya Monduli ina ukubwa wa eneo la kilometa za mraba 6,419 na jumla ya watu 182,275 kwa mwaka 2018 kwa maoteo ya sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012. Idadi ya watu inaongezeka kwa asilimia 2.7 kwa mwaka. Ina tarafa 3, kata 20 na vijiji 62.

Taarifa mafanikio ya Miaka 3 tangu serikali ya awamu ya tano ingie madarakani 2015/16 hadi Desemba, 2018 inatokana na juhudi za pamoja za Serikali Kuu, Wananchi wote, Viongozi wa Wilaya ngazi zote na Wadau mbalimbali wa Maendeleo walioshiriki kuchangia michango ya hali na mali pamoja na maarifa katika mchakato wote wa utekelezaji, uendelezaji na usukumaji wa maendeleo ya Wilaya kwa ujumla.

2.0 Mafanikio kwa mhutasari kisekta

Wilaya imefanikisha utekelezaji huu kwa kuzingatia Ibara zilizoanishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa awamu ya (5) yaani (2015 – 2020) utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ulielekezwa zaidi katika kuboresha miundombinu, ukusanyaji wa Mapato ya Serikali na utoaji wa huduma katika Sekta za Barabara, Elimu ya Msingi na Sekondari, Mifumo ya umwagiliaji (Kilimo), kuweka misingi ya Utawala bora, kuongeza rasilimali watu katika Sekta muhimu za utoaji wa huduma (Elimu, Afya, Maji, Kilimo/Mifugo na Sekta zinginezo).

3.0 SEKTA YA RASILIMALI WATU

Mafanikio yaliyopatikana katika idara ya Utawala na Utumishi katika kipindi mwaka 2015 hadi mwaka 2018 ni kama ifuatavyo;

- ✓ Katika kuboresha usimamizi wa rasilimali watu; Halmashauri ilifanikiwa kuwaondoa watumishi hewa 24, watumishi wenye vyeti feki na utata 52 na watumishi wasiokuwa na sifa za kimuundo 12, hivyo serikali kuokoa fedha kiasi cha **Tsh. 54,798,300.**

- ✓ Aidha watumishi **472** wameajiriwa kuanzia 2015/16 hadi 2018/19 katika sekta za Elimu msingi, Elimu sekondari, afya, watendaji wa vijiji, madereva na Utawala. Mchanganuo wa idadi ya watumishi kisekta ni idara ya afya watumishi 65, idara ya elimu msingi na sekondari watumishi 323, watendaji wa vijiji 36, madereva 6 na idara ya utawala watumishi 42.

- ✓ Katika kipindi cha mwaka 2015 hadi 2018 watumishi waliopandishwa madaraja ni 334 hii imeongeza morali ya kazi kwa watumishi.

- ✓ Hadi kufikia mwaka 2018/2019 jumla ya watumishi 84 wamepata fursa za kwenda masomoni kusoma fani mbalimbali, hii itawezesha ufanisi wa kazi kuongezeka pindi watakapo rejea kutoka masomoni na kuitumikia Serikali.

- ✓ Katika kipindi cha hadi kufikia 2018/2019 serikali imeweza kulipa madeni ya watumishi jumla ya Tsh. 160,728,744.00/= yameshalipwa kwa watumishi mbalimbali. Madeni haya yanajumuisha madeni ya mapunjo ya mishahara pamoja na madeni ya likizo za walimu.

- ✓ Kwa mwaka 2015/2016 bajeti ya mishahara ilikuwa ni Tsh. 16,927,660,100 na kwa mwaka 2018/2019 bajeti ya mishahara ni 17,721,017,000 ongezeko hili linatokana na ajira mpya 472 na waliopandishwa madaraja.

4.0 SEKTA YA ELIMU SEKONDARI

Idara ya elimu sekondari ina shule 12 za serikali na shule 10 zisizo za serikali. Kati ya shule hizo shule 5 zikiwemo 2 za serikali na 3 za binafsi zina kidato cha tano na sita na shule. Jumla ya wanafunzi katika shule za serikali ni **7,251** wavulana 3,546 wasichana 3,705. Kwa upande wa shule zisizo za serikali zina jumla ya wanafunzi **2,139** ikiwa wavulana 819 na wasichana 1,320. Hivyo kufanya jumla ya wanafunzi wote wa sekondari kuwa **9,390**

Aidha shule za sekondari za serikali zina jumla ya walimu 389 wakiwemo stashahada 146, shahada 236 na shahada ya uzamili 07.

Mafanikio katika idara ya elimu sekondari kwa kipindi cha miaka 3 ni kama inavyoonekana hapa chini;

4.1 Kuongezeka kwa Idadi ya Wanafunzi

Kutokana na mpango wa Elimu bila malipo, idadi ya wanafunzi imeongezeka kutoka wanafunzi 6,711 mwaka 2015 hadi kufikia wanafunzi 7,251 mwaka 2018 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 8.04.

4.2 Ajira ya Walimu wa Masomo ya Sayansi

Serikali ya awamu ya tano imeendelea kuhakikisha kuwa masomo ya sayansi na hisabati yanafundishwa kikamilifu kwa kuajiri walimu wa masomo hayo. Kwa mwaka 2017 waliajiriwa walimu 08 na mwaka 2018 waliajiriwa walimu 05 hivyo kufanya jumla walimu walioajiriwa kati ya mwaka 2015 na 2018 kufikia walimu 13.

4.3 Mpango wa Elimu Bila Malipo

Mpango huu umeanzishwa mwaka 2016 ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wanahudhuria shule bila kubughudhiwa kwa kurudishwa nyumbani kwa kutolipiwa ada au kudaiwa michango mbalimbali ya shule. Serikali imekuwa ikitoa fedha za chakula kila mwaka katika shule 12 za serikali za bweni zilizopo katika wilaya ya Monduli.

Kwa miaka yote mitatu idara ya elimu sekondari imepokea jumla ya Tshs.12,919,711,548 ambapo kati ya fedha hizi Tshs 4,069,800,821.00 ni fidia ya ada, Tshs 8,487,669,853.00 ni fedha za chakula na Tshs 362,240,874.00 ni fedha za uendeshaji (capitation) haya ni mafanikio makubwa. Jedwali lifuatalo linafafanua mapokezi ya fedha za mpango wa Elimu Bila Malipo:

Jedwali kuonesha mapokezi yafedha za elimu bila malipo;

Na.	MAHITAJI	2016	2017	2018	ONGEZEKO	% YA ONGEZEKO
1	FIDIA YA ADA	1,407,840,000	1,388,849,124	1,273,111,697	-134,728,303	-9.57
2	CHAKULA	2,665,236,000	2,630,504,860	3,191,928,993	526,692,993	19.76
3	UENDESHAJI	132,684,000	131,041,760	98,515,113	-34,168,887	-25.75
4	POSHO YA MADARAKA	3,600,000	3,600,000	3,600,000	-	-

Mapokezi haya ya fedha katika shule zetu yameimarisha mahudhurio ya wanafunzi, yameboresha uwepo wa vifaa vya kujifunzia na kufundisha na wakuu wa shule wameendelea kuboresha utendaji wao wa kazi.

4.4 Kubaini Wanafunzi Hewa

Zoezi la kubaini wanafunzi hewa lilifanyika katika idara ya elimu sekondari na kubaini wanafunzi 155. Zoezi hili limeongeza umakini katika kushughulikia taarifa za wanafunzi na hivyo kupunguza gharama kwa serikali katika kugharamia wanafunzi katika mpango wa elimu bila malipo.

4.5 Kuimarika kwa Matokeo ya Mitihani ya Taifa;

Ufaulu wa wanafunzi katika mitihani ya taifa ya kidato cha Nne umekua ukiongezeka ambapo mwaka 2015 ufaulu ulikuwa 69.1% .Mwaka 2016 ufaulu ulifikia 88.81% na mwaka 2017 ufaulu ulikuwa ni 87.82%.

Jedwali.No:4 Hali ya ufaulu wa CSEE- kwa miaka mitatu (2015-2017)

Mwaka	Waliofanya			Daraja I-III			Daraja IV			Walioshindwa		
	WV	WS	JML	WV	WS	JML	WV	WS	JML	WV	WS	JML
2017	835	799	1634	315	198	513	437	485	922	83	116	199
%				19	12	31	27	30	57	5	7	12
2016	783	806	1689	327	297	624	386	479	865	79	122	200
%				19.3	17.6	36.9	22.8	28.4	51.2	4.7	7.2	11.9
2015	916	1023	1939	283	170	453	419	488	907	194	359	573
%				**15**	**9**	**24**	**20.8**	**25**	**45.8**	**11.2**	**19**	**30.2**

Kwa kidato cha sita ufaulu wa wanafunzi katika mitihani ya taifa Mwaka 2016 ulifikia 99% na mwaka 2017 ufaulu ulikuwa ni 98% na kwa mwaka 2018 ufaulu ulikuwa asilimia 99.4.

Jedwali.No:5 Hali ya ufaulu wa ACSEE-kwa miaka mitatu (2016-2018)

Mwaka	Waliofanya			Daraja I-III			Daraja IV			Walioshindwa		
	WV	WS	JML	WV	WS	JML	WV	WS	JML	WV	WS	JML
2018	146	207	353	142	202	344	4	3	7		2	2
%				40.2	57.3	97.5	1.1	0.8	1.9	0	0.6	0.6
2017	126	128	254	119	118	237	10	7	17	0	3	3
%				47	46	93	4	2.6	6.6	0	0.4	0.4
2016	144	119	263	138	112	250	4	5	9	2	2	2
%				**52**	**43**	**95**	**1.5**	**1.9**	**3.4**	**0.8**	**0.8**	**1.6**

4.6 Miundo Mbinu ya Shule

Miundombinu ya shule imeendelea kuimarika kutokana na jitihada za serikali pamoja na uchangiaji wa jamii katika maendeleo ya shule zao. Jedwali hapa chini linaonesha ongezeko la miundombinu ya shule za sekondari za serikali.

Jedwali kuonesha miundombinu ya shule;

S/N	AINA YA MUUNDOMBINU	2015	2018	0NGEZEKO	% YA ONGEZEKO
1	Mabweni / hostel	52	61	9	17.31
2	Nyumba za walimu	91	101	10	10.99
3	Vyumba vya maabara	14	23	9	39.13
4	Madarasa	149	156	7	4.70
5	Matundu ya vyoo	241	290	49	16.90
6	Vitanda	4720	5060	340	7.20
7	Meza naviti	6711	7251	540	8.05

Aidha kutokana na ongezeko kubwa la ufaulu wa wanafunzi wa darasa saba mwaka 2018, jamii imehamasika vya kutosha kuhakikisha kuwa miundombinu ya kutosha kupokea wanafunzi wote waliofaulu kuingia kidato cha kwanza mwaka 2019 inajengwa na inakamilika kwa wakati. Ili kukidhi mahitaji hayo ya miundombinu, yapo madarasa 19 na mabweni 12 yanayojengwa katika shule zetu na yamefikia hatua mbalimbali za ujenzi.

4.7 Mifumo ya Kielektroniki

Katika kipindi cha 2015 hadi 2018 imeanzishwa mifumo ya kiielectroniki ambayo inasaidia sana katika utoaji wa taarifa. Mifumo wa kwanza ni Basic Education management Information System (BEMIS). Mfumo huu umerahisisha sana ukusanyaji wa takwimu mbalimbali na unaokoa muda na fedha. Mfumo wa pili ni “Facility Financial Accounting Reporting System” (FFARS) mfumo huu umerahisha sana utoaji wa taarifa za kifedha kutoka katika shule zetu.

Mifumo yote miwili inatuunganisha na wizara ya Ofisi ya Rais TAMISEMI hivyo kuongeza uwazi katika utoaji wa taarifa mbalimbali.

4.8 Ongezeko la Shule za Sekondari

Kwa kipindi cha mwaka 2015 hadi 2018 zimeongezeka shule mbili (2) zisizo za serikali hivyo kuongeza shule zisizo za serikali kutoka 8 hadi 10 shule hizo ni Tumaini Senior shule ya sekondari iliyopo Makuyuni na Alfa Omega shule ya sekondari ilioyopo Monduli Mjini. Shule hizi zimeongeza wigo wa kutoa elimu kwa jamii katika wilaya yetu. Aidha kuna shule moja ya sekondari ya serikali inayoendelea kujengwa katika kata ya Mswakini.

5.0 SEKTA YA ELIMU MSINGI

Wilaya ya Monduli ina shule za msingi za serikali **63** na shule zisizo za serikali 15 hivyo kufanya jumla ya shule zote kuwa 78 kati ya shule za serikali shule 3 ni za bweni. Hadi kufikia Septemba 2018 idadi ya wanafunzi kuanzia darasa la awali hadi darasa la saba kwa shule za serikali ni **32,954** wakiwa ni wavulana **16,683** na wasichana **16,271.** Kwa shule za binafsi jumla ya wanafunzi ni **2,503** wavulana wakiwa ni **1,201** na wasichana **1,302.** Aidha Wilaya ina vituo vya ufundi stadi vitano, vitatu ni vya binafsi na viwili ni vya Serikali. Yapo madarasa 24 ya MEMKWA yenye wanafunzi 413, na MUKEJA madarasa 13 yenye wanafunzi 460. Shule za Msingi za serikali zina jumla ya walimu 722 ambapo walimu 550 ni wa ngazi ya cheti, 91 wa stashahada na 81 wana shahada.

5.1 Mafanikio ya Kielimu

Wilaya ya Monduli imepata mafanikio makubwa sana ya kielimu katika maeneo yafuatayo-:

5.2 Mapokezi ya Fedha

Kuanzia mwezi Desemba 2015 Utekelezaji wa ahadi ya Mhe. Rais juu ya Elimu Bila malipo ulianza kwa kupokea fedha kama ilivyooneshwa kwenya jedwali

Jedwali: No.1: Taarifa za Mapokezi ya Fedha za Ruzuku ya Uendeshaji, Chakula cha Bweni na Posho ya Madaraka Mlinganisho Mwaka 2015 na 2016- 2018.

S/N	MAHITAJI	MWAKA WA FEDHA				
		Julai-Nov.2015 (awamu ya 4)	Des 2015 hadi Juni 2016	Julai 2016-Juni2017	Julai 2017-Juni-2018	Jumla ya kuanzia Des.2015-Oktoba-2018
1	Ruzuku ya Uendeshaji	13,387,000	105,883,000	164,577,405	155,965,376	478,789,840
2	Chakula shule za bweni	381,420,000	491,817,000	948,156,753	926,144,080	2,659,145,018
3	Posho ya Madaraka	-	-	201,600,000	201,600,000	470,400,000
	JUMLA KUU	**394,807,000**	**597,700,000**	**1,314,334,140**	**1,283,709,455**	**3,608,334,858**

Aidha Idara ya elimu Msingi ilipokea tena jumla ya fedha **Tsh 148,900,478.76** kwa ajili ya mradi wa ***Lipa kadiri ya Matokeo (EP4R***) ambapo Tsh. 22,629,857.00 mwaka (2015/16) Tsh. 39,803,359.44 mwaka (206/17) na Tshs. 86,467,262.32 mwaka (2017/18). Fedha za EP4R zilitumika kujenga miundombinu ambayo ni vyumba vipya vya madarasa 6 ukarabati madarasa 3 umaliziaji madarasa 3, ujenzi wa nyumba 2 za walimu na ujenzi wa matundu 16 ya vyoo pia zilitumika kwenye ukusanyaji wa takwimu za kielimu na kusawazisha ikama ya walimu ambapo kwa wilaya ya Monduli ilihamisha walimu 80 kutoka shule za Sekondari kwenda shule za msingi.

Serikali ilitoa tena **Tsh.82,124,618.00** kwa kipindi cha 2016-2018 kupitia Mpango wa Uimarishaji wa Stadi za KKK (LANES) zikiwa ni za uendeshaji wa mafunzo ya kamati za shule 59 na ufuatiliaji wa Mpango wa Uimarishaji wa Stadi za KKK shuleni.

5.3 Ongezeko la uandikishaji wa wanafunzi darasa la awali na darasa la I na ujenzi wa shule mpya (2015-2018)

Kwa kipindi cha miaka mitatu kumekuwa na ongezeko la ujenzi wa shule mpya 7 na kuongeza shule kutoka 67 (2015) hadi shule 78 (2018) sawa na ongezeko la 14.1%. Uandikishwaji wa wanafunzi wa darasa la awali na darasa la kwanza nao umekuwa ukiongezeka kila mwaka, Ongezeko hili linatokana na sera ya Elimu msingi bila malipo kama ilivyooneshwa kwenye jedwali.

Jedwali *No:2 Uandikishwaji wa Wanafunzi Darasa la Awali na la I Mwaka 2016- 2018*.

DARASA	MWAKA	MATAZAMIO			WALIOANDIKISHWA			ASILIMIA
		WAV	WAS	JML	WAV	WAS	JUML	
AWALI	2015	2104	2062	4166	1517	1448	2965	71.2
	2016	2238	2096	4334	1844	1757	3601	83
	2017	2042	2018	4060	2123	2022	4145	102.1
	2018	2122	1910	4032	2130	1930	4060	101
DARASA LA 1	2015	2509	2510	5019	2395	2393	4788	95.39
	2016	2979	2902	5881	3216	2991	6207	106
	2017	2769	2708	5477	3005	2879	5884	107.4
	2018	2689	2551	5240	3126	3012	6138	117

5.4 Kuongezeka kwa Ufaulu wa Mitihani ya Kitaifa

Kwa kipindi cha miaka 3 (2016-2018) kumekuwepo na kupanda kwa asilimia ya ufaulu wa mitihani ya kumaliza darasa la Saba (PSLE) mwaka hadi mwaka kama ilivyooneshwa kwenye majedwali.

Jedwali.No:3 Hali ya Ufaulu wa Darasa la Saba kwa Miaka Mitatu(2015-2017)

Mwaka	Waliofanya mtihani			Waliofaulu			Asilimia
	WV	WS	JML	WV	WS	JML	
2015	1231	1438	2669	894	985	1879	70.401
2016	1255	1417	2672	898	1018	1916	71.707
2017	1506	1546	3052	1087	1045	2132	69.86
2018	1448	1638	3086	1213	1415	2628	85.16

5.5 Utekelezaji wa Mpango wa Kukuza Stadi za KKK

Katika kipindi cha mwaka 2016 hadi 2018 Serikali ya awamu ya 5 ilianza kutekeleza mpango wa kukuza stadi za KKK ambapo ilijikita katika kujengea walimu stadi na mbinu mpya za kufundisha na kusimamia ufundishaji wa KKK. Walimu 372 walipata mafunzo hayo wakiwa ni-; walimu wa awali hadi darasa la 4, walimu wakuu na waratibu elimu kata. Aidha Wajumbe 728 wa kamati za shule walipata mafunzo juu ya usimamizi wa shule. Hii imepelekea kuwepo na mabadiliko ya ufundishaji kwa kutumia zana ambapo shule zote zina madarasa ya awali, 1 na 2 yanayoongea.

Jedwali No.4: ***Idadi ya Walimu Waliopata Mafunzo ya KKK 2016-2018***

Idadi ya shule	Walimu drs Awali	Walimu Drs 1&2	Walimu Drs 3&4	Walimu wakuu	Waratibu E/Kata	Jumla
59	59	118	116	59	20	372

Hadi kufikia Novemba 2018 hali ya wanafunzi wa darasa la 1 hadi la 3 waliomudu stadi za KKK katika wilaya ni nzuri kwani ni 92% ya wanafunzi wa darasa la 1-3 walikuwa wameshamudu stadi za KKK ukilinganisha na mwaka 2015 ilikuwa ni 89%. Mchanganuo kimadarasa ni kama ilivyooneshwa kwenye jedwali.

Jedwali *No.5 Idadi ya Wanafunzi Darasa la 1 hadi 3 Wanaomudu stadi za KKK hadi Novemba 2018*

DARASA	**WALIOSAJILIWA**			**WASIOJUA KKK**			
	WV	**WS**	**JM**	**WV**	**WS**	**JM**	**%**
I	3447	3274	6721	2985	2864	5849	88
II	3139	3042	6181	2853	2807	5660	91.6
III	2494	2338	4832	2403	2273	4676	96.8
JUMLA	**9080**	**8654**	**17734**	**839**	**710**	**1549**	**92**

5.6 Ununuzu wa Vifaa vya Usafiri (Pikipiki) kwa maafisa Elimu kata na kompyuta.

Katika kutekeleza mpango wa Ukuzaji wa stadi za KKK serikali kupitia mpango wa LANES ulinunua pikipiki 20 kwa Maafisa Elimu Kata ambazo wanazitumia kufanya ufuatiliaji wa ufundishaji shuleni vyombo hivyo viliigharimu serikali Tshs 59,999,980. Aidha serikali ilisambaza seti 3 za kompyuta, meza na viti kwa Wilaya ya Monduli.

5.7 Kuboreshwa na Kuongezeka kwa Miundombinu ya Elimu

Kwa kipindi cha miaka 3 Serikali imeondoa kabisa upungufu wa madawati katika shule zote za msingi kwenye wilaya ya Monduli ambapo Juni 2015 kulikuwa na Upungufu wa madawati 2,456 na ilipofika Januari 2018 upungufu wa madawati ulikuwa ni 0

Jedwali *No: 6 Idadi ya Miundombinu ya Kufundishia na Kujifunzia ilivyoongezeka toka 2016 hadi 2018*

Aina	**Mwaka 2015**	**Mwaka 2016**	**Mwaka 2017**	**Mwaka 2018**
Madawati	7268	12177	12196	12196
Nyumba	195	213	218	223

Aina	Mwaka 2015	Mwaka 2016	Mwaka 2017	Mwaka 2018
Madarasa	444	482	477	481
Vyoo	520	653	681	688

5.8 Mapokezi ya Vitabu vya Kiada na Ziada

Kwa kipindi cha mwaka 2016 hadi 2018 Serikali ya awamu ya 5 ilisambaza vitabu vya kiada na ziada katika shule 59 na kufikia uwiano wa kitabu 1 kwa wanafunzi 3 (1:3) kwa baadhi ya madarasa na 1:4 kama ilivyooneshwa kwenye jedwali.

Jedwali kuonesha idadi ya Vitabu vilivyosambazwa shuleni na serikali 2016-18

Mwaka	darasa	Aina ya vitabu		
		kiada		Ziada/hadithi
		idadi	Uwiano kitabu kwa wanafunzi	
2016-18	1	34,799	1:3	4,766
	2	22,216	1:3	4,766
	3	27,678	1:4	4,766
	4	15,158	1:1	4,766
	5	9,004	1:4	0
	JUMLA	108,855		19,064

5.9 Uanzishwaji wa Mifumo ya Kielektroniki ya Taarifa za Kielimu.

Kwa kipindi cha mwaka 2016-18 Serikali ya awamu ya 5 ilianzisha mifumo ya kukusanyia takwimu za kielimu (Basic Education Management Information Systeam-BEMIS) na mfumo wa usajili wa wanafunzi kuanzia darasa la 1 hadi la 7 na kupewa namba ya kipekee (Unique Identification Number) itakayomtambulisha katika ngazi zote za kielimu (Primary Records Manager-PReM) mifumo hii imerahisisha sana upatikanaji wa takwimu na taarifa za wanafunzi kwa wadau wa elimu na kuondoa tatizo la wanafunzi hewa pamoja na kughushi vyeti na majina kwenye mfumo wa elimu.

6.0 SEKTA YA AFYA

Mwaka 2015 Wilaya ya Monduli ilikuwa na jumla ya vituo vya kutolea huduma 37; Zahanati 35; 30 za serikali, 5 za binafsi, kituo cha afya 1cha serikali, 1 cha binafsi na hospitali moja ya Wilaya.

Mwaka 2018 Wilaya ina jumla ya vituo vya kutolea huduma 45. Zahanati za serikali 36, na Zahanati binafsi 4, vituo vya afya vya serikali ni 2, vituo vya binafsi 2 na hospitali ya Wilaya moja. Ongezeko ni vituo vya kutolea huduma 8; zahanati 6, kituo cha afya cha serikali 1 na cha binafsi 1

Vilevile, katika kuboresha huduma za upasuaji kwa ajili ya kuimarisha afya ya wazazi na watoto, Serikali imetoa fedha kwa ajili ya ujenzi/ukarabati wa vituo viwili vya afya ambavyo ni Makuyuni na Mto wa Mbu. Jumla ya ufadhili huo ni **Tsh. 800,000,000**, ikiwa **Tsh. 400,000,000** kwa kila kituo. Kwa kutumia fedha hizo, tumeweza kujenga majengo yafuatayo-:

- **KITUO CHA AFYA MTO WA MBU;** Jengo la upasuaji**,** Nyumba ya mtumishi**,** Jengo la kufulia**,** Jengo la x-ray na ultra sound**,** Jengo la maabara**,** Jengo la wazazi na Ukarabati wa jengo la wagonjwa wa Nje.

Majengo haya yote yamekamilika na yameanza kutumika kwa awamu. Kuanza kutumika kwa majengo haya kumeboresha sana hali ya upatikanaji na ubora wa huduma za afya.

- **KITUO CHA AFYA MAKUYUNI;** Jengo la wagonjwa wa nje**,** Jengo la upasuaji**,** Jengo la wazazi na Jengo la mtumishi.

Ujenzi huu umefikia hatua ya umaliziaji na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Januari. Kukamilika kwa majengo haya kutaboresha sana huduma za afya hasa zinazolenga wazazi na watoto.

Nyumba za Watumishi; Katika vituo vyote vya kutolea huduma zilikua 45 kwa mwaka 2015 na zimeongezeka na kufikia 53 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 17.

6.1 Dawa na Vifaa Tiba

Bajeti ya dawa imeongezeka kutoka Tsh. 176,289,157 mwaka 2015 hadi Tsh. 567,526,288 kwa mwaka 2018 sawa na ongezeko la asilimia 221.9. Upatikanaji wa dawa na vifaa tiba umezidi kuimarika katika vituo vya kutolea huduma ambapo mwaka 2015 kiwango cha upatikanaji kilikuwa ni asilimia 75 na Disemba 2018 kimefikia asilimia 98.2%

Idadi ya vituo vya serikali vilivyopokea mgawo wa dawa kupitia bohari kuu ya dawa imeongezeka kutoka vituo 32 mwaka 2015 hadi vituo 37 mwaka 2018.

Jedwali 1; Hali ya upatikanaji wa dawa na vifaa tiba 2015- 2018

MWAKA	BAJETI YA DAWA NA VIFAA TIBA
2015	176,289,157
2016	292,535,134
2017	513,041,346
2018	567,526,288

6.2 Chanjo

Kwa mwaka 2015 Wilaya ya Monduli ilikua na vituo 33 vinavyotoa huduma za chanjo sawa na asilimia 86.8 % na mwaka 2018 vituo vimeongezeka na kufikia jumla ya vituo 40 vinatoa huduma za chanjo sawa na asilimia 89 ya vituo vyote vinavyotoa huduma ndani ya Wilaya. Aidha, tumeanzisha chanjo mpya ya saratani ya shingo ya kizazi kwa wasichana wa umri wa miaka 14. Chanjo hii ni kinga thabiti dhidi ya saratani ya shingo ya kizazi.

Jedwali 2; Hali ya chanjo

MWAKA	BCG	PENTA 3	SURUA 1	PCV 3	HPV 1	IDADI VITUO VINAVYOTOA CHANJO
2015	96%	96%	71%	98%	0%	33
2016	106%	108%	82%	108%	0%	36
2017	119%	118%	117%	118%	0%	37
2018	133%	124%	124%	124%	73%	40

6.3 Afya ya Uzazi na Mtoto

Katika Wilaya ya Monduli mwaka 2015 vituo vilivyokua vinavyotoa huduma ya afya ya mama na mtoto vilikuwa 33 na sasa vimeongezeka na kufikia 38 mwaka 2018 sawa na asilimi 84.4 ya vituo vyote vya kutolea huduma za afya.

6.4 Kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi

Kiwango cha Vifo vitokanavyo na uzazi vimepungua toka 161/100,000 mwaka 2015 na kufikia 87/100,000 mwaka 2018 sawa na asilimia 54 (54%). Mafanikio haya yanatokana na ongezeko la vituo vya kutolea huduma.

6.5 Kupungua kwa vifo vya watoto walioko chini ya umri wa miaka mitano

Kiwango cha vifo vya watoto chini ya miaka 5 vimepungua kutoka 77/1000 kwa mwaka 2015 hadi 17/1000 kwa mwaka 2018 sawa na asilimia 22.1.

Jedwali 3; Kupungua kwa vifo vitokanavyo na uzazi

MWAKA	VIFO VYA WATOTO CHINI YA MIAKA 5	VIFO VITOKANAVYO NA UZAZI
2015	77/1000	161/100,000
2016	101/1000	132/100,000
2017	42/1000	111/100,000
2018	19/1000	87/100,000

6.6 Wanaojifungua Vituoni

Kiwango cha wajawazito wanaojifungulia katika vituo vya kutolea huduma za afya kimeongezeka toka wajawazito 2231 sawa na 32% mwaka 2015 na kufikia 3,150 sawa na 45% mwaka 2018.

6.7 Mahudhurio ya Kliniki ya Wajawazito

Kiwango cha wajawazito wanaotimiza mahudhurio manne ya msingi kimeongezeka toka wajawazito 3,336 sawa na 40% mwaka 2015 na kufikia wajawazito 3,867 sawa 56% mwaka 2018

6.8 Matumizi ya huduma za uzazi wa mpango

Kiwango cha matumizi ya njia za kisasa za uzazi wa mpango kimeongezeka toka wazazi 16,050 sawa na 27% mwaka 2015 na kufikia wazazi 20,450 sawa na 53% mwaka 2018

6.9 Uchunguzi wa Saratani ya mlango wa kizazi

Idadi ya akina mama waliofanyiwa uchunguzi wa saratani ya mlango wa kizazi imeongezeka kutoka 536 kwa mwaka 2015 na kufikia 2,877 kwa mwaka 2018.

Jedwali 4: Mahudhurio ya kliniki, kujifungua katika vituo vya afya, uzazi wa mpango na uchunguzi wa saratani ya mlango wa kizazi

MWAKA	ASILIMIA YA MAUDHURIO MANNE YA MSINGI	ASILIMIA YA WANAOJIFUNGULIA KWENYE VITUO VYA AFYA	MATUMIZI YA UZAZI WA MPAMGO WA KISASA	IDADI YA WANAWAKE WALIOFANYIWA UCHUNGUZI WA SARATANI YA MLANGO WA KIZAZI
2015	40%	32%	27%	536
2016	44%	38%	44%	631
2017	52%	41%	38%	1587
2018	56%	45%	53%	2877

6.10 Maambukizi ya Virusi vya UKIMWI:

Hali ya maambukizi ya VVU na UKIMWI Wilaya Monduli imezidi kupungua kutoka wagonjwa wenye maambukizi 528/13,047 sawa na asilimia 4% 2015 hadi wagonjwa wenye maambukizi 557/51,729 sawa asilimia 1.1% 2018. Hii ni kutokana na jitihada mahususi zinazofanywa na wadau mbalimbali ikiwepo kampeni ya uhamasishaji na upimaji wa VVU katika ngazi ya jamii na katika vituo vya kutolea huduma. Baadhi ya kampeni za kitaifa zinazotekelezwa na Wilaya ya Monduli ni pamoja na kampeni ya “FURAHA YANGU” PIMA JITAMBUE ISHI.

Jedwali 5; Hali ya maambukizi ya VVU na UKIMWI 2015 -2018

MWAKA	IDADI YA WALIOPIMWA VVU	IDADI YA WALIOGUNDLIKA KUWA NA MAAMBUKIZI MAPYA VVU	ASILIMIA YA MAAMBUKIZI MAPYA YA VVU
2015	13047	528	4%
2016	13349	517	3.80%
2017	17452	497	2.80%
2018	51729	557	1.10%

6.11 Ugonjwa wa Malaria

Hali ya ugonjwa wa Malaria imezidi kupungua katika Wilaya ya Monduli ambapo 2015 ugonjwa huu ulikuwepo kwa asilimia 3% hadi kufikia 2018 imefika 0.1%. Ambapo kwa ukanda huu tumengia kwenye kundi linaloelekea kutokomeza ugonjwa wa Malaria. Ziko jitahada kubwa zikiwemo ugawaji wa viuwa wadudu na ugawaji wa vyandarua.

Jedwali 6; Hali ya ugonjwa wa Malaria

MWAKA	ASILIMIA YA UWEPO WA UGONJWA WA MALARIA
2015	3%
2016	2.20%
2017	1%
2018	0.10%

6.12 Hali ya Mfuko wa CHF

Hali ya mfuko wa Afya ya jamii (CHF) imeendelea kuimarika kutoka kaya 5,297 sawa na asilimia 16% kwa mwaka 2015 hadi kufikia kaya 12,065 sawa asilimia 36% kwa mwaka 2018 zilizojiunga na mfuko wa CHF. Hii ni kwa sababu ya uwepo wa dawa katika vituo vya kutolea huduma jambo ambalo linawatia wananchi hamasa ya kujiunga na mfuko wa Afya ya Jamii kwani wana uhakika wa kupata dawa.

Vilevile, Serikali imeanzisha bima ya afya ya jamii iliyoboreshwa (Improved CHF) ambayo itakuwa msaada mkubwa kwani imeongeza idadi ya huduma atakazonufaika nazo mchangiaji na kuongeza wigo kwa mnufaika kwani itatumika tangu zahanati hadi hospitali za mikoa.

Jedwali 7; Hali ya mfuko wa CHF

Mwaka	Asilimia ya ongezeko wanachama wanaojiunga kwenye mfuko wa CHF
2015	12%
2016	16%
2017	29%
2018	36%

6.13 Huduma kwa Makundi Maalum

Kuendelea kutoa huduma kwa makundi maalum, kwa kutoa vitambulisho vya huduma za matibabu bure kwa wazee 3,575 kati ya 7,789 sawa na 46%. Mabaraza ya wazee yameundwa katika kata zote 20 na Vijiji 62 pamoja na baraza 1 katika ngazi ya Wilaya. Kamati za Ulinzi wa mwanamke na mtoto zimeundwa katika Vijiji 62, Kata 20, na 1 katika ngazi ya Wilaya. Kwa mwaka 2015 tulikuwa na chama 1 cha watu wenye ulemavu wa ngozi (TAS- Tanzania Albinism Society) na 2018 kuna vyama 5 vya watu wenye ulemavu wa ngozi, viziwi na wasioona, tumefanikiwa kugawa Vifaa mbalimbali kwa watu wenye ulemavu (Mafuta maalum ya ngozi kwa watu wenye ulemavu wa ngozi, miwani na kofia).

Vile vile utambuzi wa watoto wanaoishi katika mazingira magumu umefanyika ambapo jumla ya watoto 7,023 wametambuliwa na watoto 2,865 wanapatiwa huduma mbalimbali na Serikali pamoja na wadau sawa na asilimia 41%.

Jedwali 8; Huduma za ustawi wa jamii

MWAKA	Vitambulisho vya wazee	Uundaji wa mabarza ya wazee	Ununuzi wa Vifaa tiba kwa watu wenye Ulemavu	Uundaji wa kamati za ulinzi mama na mtoto	Utambuzi wa watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu	Vyama vya watu wenye Ulemavu
2015	0	0	0	0	357	0
2016	1027	0	9	79	791	1
2017	2548	79	10	79	2865	3
2018	3575	83	30	83	2869	5

7.0 SEKTA YA MAENDELEO YA JAMII

Idara ya Maendeleo ya Jamii, Ustawi wa Jamii na Vijana imegawanyika katika sehemu tatu kuu yaani; Maendeleo ya Jamii, Ustawi wa Jamii na Vijana Idara inaratibu shughuli mbalimbali za jamii ambazo ni mtambuka hivyo inatekeleza kazi za jamii kawa kushirikiana na wadau hivyo kuleta mabadiliko ya kimaendeleo kwenye shughuli za idara kwa kuratibu na kusimamia vikundi vya wajasiriamali na makundi maalum.

Mafanikio yaliyofikiwa kwa kipindi cha 2016 hadi 2018;

- ✓ Halmashauri imewajibika kuratibu vikundi vya wanawake na vijana kwa kuhakikisha vinapata usajili ili viweze kupata fursa ya mikopo, kwa mwaka 2015 jumla ya vikundi 206 vyenye wanachama 3,950 vilitambuliwa na kupata usajili. Kwa mwaka wa 2016 hadi 2018 vikundi vya kiuchumi vya wanawake 471 na vijana 63 vyenye jumla ya wanacha 13,450 vimepewa usajili wa ndani hii ni sawa na ongezeko la asilimia 38.5.

- ✓ Halmashauri katika kuhakikisha kuwa inaendelea kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu, elimu ya ujasiriamali na biashara ili kuwawezesha kuongeza ajira, ujuzi wa kujiajiri, fursa za kipato na kujikimu. Imeweza kuchangia kwenye mfuko wa wanawake na vijana. Ukilinganisha na kipindi cha mwaka 2015 ambapo uchangiajia ulikuwa asilimia 5 kwasasa kuna ongezeko la uchangiaji kwa asilimia 60, kama jedwali linavyojieleza;

Na	**Mwaka**	**Asilimia 10 ya mapato ya ndani yaliyopelekwa kwenye mfuko.**	**Asilimia**
1.	2015/2016	25,000,000	27%
2.	2016/2017	115,249,273	90%
3.	2017/2018	66,000,000	56%
4.	Julai hadi Disemba 2018	40,000,000	32%
	Jumla	**246,249,273**	

- ✓ **Mikopo kwa vikundi vya wanawake na vijana;** kwa mwaka 2015 Jumla ya shilingi 63,724,500 zilikopeshwa kwa vikundi vya akina mama na vijana kwa mchanganuo ufuatao; akina mama shilingi 40,724,5000 jumla ya wanaufaika 380 na vijana shilingi 23,000,000 wanufaika 88. Aidha kwa mwaka 2016 hadi 2018 Jumla ya Shilingi 430,400,000.00. zimekopeshwa kwa Vikundi 109 vya wanawake na Vijana pamoja na walemavu vyenye wanufaika 1,545 kwa mchanganuo ufuatao; akina mama shilling 284,000,000 wanufaika 1,200 (Vikundi 69) na vijana shilling 146,400,000 wanufaika 585(Vikundi 39) na walemavu shilingi 3,000,000.00 Wanufaika 22 (Kikundi1) Fedha hizo ni sawa na ongezeko la shilingi 366,675,500 sawa na asilimia 85. Fedha zilizokopeshwa ni mchango wa Halmashauri na fedha zilizokuwa kwenye mfuko wa wanawake na vijana. Mwaka 2017 Serikali kuu imeipatia wilaya Tsh 54,000,000 kwa ajili ya kuwakopesha vijana. Fedha hizi zimewafikia vikundi 10 vya vijana vyenye wanufaikaji 95.
- ✓ Zoezi la uhakiki wa mashirika yasiyo ya Kiserikali Wilayani – NGOs, CBOs, na FBOs. Mwaka 2015 kanzi data ya mashirika ilionyesha kuwa kuna mashirika 52 yanayofanyakazi Wilayani Monduli. Katika zoezi la uhakiki wa mashirika lililoratibiwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto lilianza rasmi Agosti 2017. Uhakiki huo uliweza kubaini na kuondoa mashirika yasiyokidhi vigezo. Baada ya uhakiki unaoendelea mashirika 33 yameonekana kufanya kazi kwa kufuata taratibu, kanuni na sheria za mashirika yasiyo ya Kiserikali. Mashirika hayo 33 yanajihusisha na shughuli zifuatazo:-
- ✓ Mashirika 9 yanatoa huduma za UKIMWI na kusaidia watoto waishio katika mazingira hatarishi, mashirika 10 yanatoa elimu za ujasiriamali kwa vikundi vya kiuchumi na utunzaji wa mazingira, shirika 1 linatoa huduma za usaidizi wa kisheria katika jamii, mashirika 4 yanatoa huduma za usimamizi bora wa ardhi, mashirika 5 yanatoa huduma za afya, mashirika 2 yanatoa huduma ya kupinga matumizi ya madawa ya kulevya, mashirika 2 yanasaidia uhamasishaji kwa jamii kupeleka watoto wa kike shuleni,

- ✓ Vikundi vya VICOBA; kwa mwaka 2015 vilikuwa VICOBA 87 vyenye mtaji wa Tsh 3,655,000,000 na wanachama 2,610 ambavyo ni sawa na asilimia 12.4, na mwaka 2018 vikundi vya VICOBA vimeongezeka na kufikia 145 vikiwa na wanachama 4,350 na mtaji wa Tsh. 6,975,000,000 ikiwa ni ongezeko la asilimia 60 usajili wa vikundi hivi unaendelea.

- ✓ Makundi Maalum; Wilaya imeratibu shughuli za makundi maalum ambapo mwaka 2016 zoezi la utambuzi wa watu wenye ulemavu 906 ulifanyika na kuwekwa kwenye mipango ya ulinzi kupitia kamati za watu wenye ulemavu kuanzia ngazi ya kijiji hadi Wilaya. Utambuzi wa wazee 7,789 umefanyika kati yao 1,108 wana vitambulisho vya kuweza kupata matibabu bure. Mwaka 2018 zoezi la utengenezaji wa vitambulisho vya wazee 2,548 limefanyika katika kata 7 vitambulisho hivyo viko katika hatua ya ukamilishaji.

8.0 IDARA YA FEDHA NA BIASHARA

Kuanzia mwaka 2015/2016 hadi 2017/2018 Idara ya fedha na Biashara imepata mafanikio yafuatayo ambayo tunaona ni mambo ya msingi ya kujivunia:-

- ✓ Halmashauri ya Wilaya ya Monduli imeendelea kupata hati safi za ukaguzi kwa miaka miwili mfululizo kuanzia mwaka 2015/2016 hadi 2016/2017. Hati ya ukaguzi kwa mwaka 2017/2018 bado haijatolewa.
- ✓ Kuongezeka kwa makusanyo ya mapato ya ndani kutoka Tshs. 2,183,799,253 ya mwaka 2015/2016 hadi kufikia mapato ya Tshs. 2,240,186,374.00 sawa na ongezeko la 2.58% Jedwali lifuatalo linaonyesha makusanyo ya mapato kuanzia mwaka 2015 hadi 2018

Mwaka	Makisio Yaliyoidhinishwa	Kiasi Kilichokusanywa	Upungufu/Ziada	Asilimia
2015/2016	2,380,000,000.00	2,183,799,253.00	196,233,747.00	91.7
2016/2017	2,457,311,004.00	2,227,146,574.00	230,164,574.00	90.6
2017/2018	2,211,206,000.00	2,240,186,374.00	28,980,374.00	101.3

- ✓ Kuanzishwa kwa Mfumo wa uhasibu na utoaji taarifa katika vituo vya kutolea huduma (FFARS). Mfumo huu umeanza kutumika kuanzia mwaka wa fedha 2017/2018 ambapo kwa sasa unatumika katika Shule za Msingi, Shule za Sekondari, Zahanati pamoja na vituo vya Afya. Kuanzishwa kwa mfumo huu kumesaidia kuanza kupeleka fedha moja kwa moja kwenye vituo vya kutolea huduma (DHFF), ambapo kwa sasa Mfumo huu umepunguza urasimu na kuboresha utoaji wa huduma za afya kwa kuimarisha uwajibikaji na uboreshaji wa uandaaji wa mipango na bajeti.
- ✓ Kuboreshwa na kuhuishwa kwa mfumo funganishi wa usimamizi wa fedha ujulikanao kama EPICOR. Mfumo wa EPICOR umeboreshwa na kuhuishwa kutoka Epicor Toleo la 9.05 ilivyokuwa mwaka 2016/2017 hadi kufikia Epicor Toleo la 10.2 Mwaka 2017/2018. Mfumo huu umeboreshwa ambapo kwa sasa unafanya kazi kwa ufanisi zaidi kuliko ilivyokuwa hapo awali. Maboresho hayo pia yamelenga na kuunganishwa na Mkongo wa mawasiliano wa Taifa ambapo Serikali imeokoa fedha nyingi iliyokuwa inayalipa makampuni binafsi yaliyokuwa yanatoa huduma za mtandao "Internet".
- ✓ Kuanzishwa kwa Mifumo mipya ya Tehama ambayo ni:-
    - Mfumo wa kieletroniki wa ukusanyaji wa mapato (Local Government Revenue Collection System) Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR TAMISEMI) mnamo mwaka 2016 imesanifu na Kutengeneza Mifumo ya kukusanya Mapato ya Ndani (Kodi na Tozo) ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Faida za mfumo huu ni kuwa inauwezo wa kutunza taarifa za walipa kodi ambazo zinawezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweka Makadirio sahihi na kusimamia ukusanyaji wa mapato kwa urahisi zaidi. Hali kadhalika, Mifumo imepelekea kuanza kwa matumizi ya Mifumo ya Kieletroniki ya Malipo – "Eletronic Payment" (Mfano Point of Sale –POS, M-PESA, Tigo PESA, Airtel Money, Zpesa, Mabenki Max Malipo n.k)
    - Usanifu na utengenezaji wa Mfumo mpya wa uandaaji mipango na bajeti (Web-based Planrep) Mfumo ulioanza kutumika kuanzia mwaka 2018/2019, kwa mwaka 2015 mfumo

uliokuwa unatumika ni “Planrep” ambayo siyo web-based. Mfumo wa Planrep pamoja na mambo mengine umeboreshwa na umeleta manufaa yafuatayo:-

- Kuwasilisha mipango na bajeti kupitia miundombinu ya TEHAMA ya OR-TAMISEMI (Auto submission) Jambo hili limepunguza gharama kwa kuwa hapo awali ilitulazimu kuzalisha nakala za kutosha za rasimu ya mpango na bajeti kwa ajili ya kupitiwa katika ngazi ya Mkoa, TAMISEMI na Hazina.
- Kuwepo na toleo moja la mfumo linalosimamiwa na OR TAMISEMI (Centralized web based Planrep)
- Kurahisisha zoezi la upitiaji wa mipango na bajeti hivyo kupunguza gharama za kuchapa vitabu
- Mfumo mpya wa Planrep una dirisha la kuingiza mipango ya ngazi za msingi za kutolea huduma (Facility level plans and budget)

9.0 MIRADI YA MAENDELEO

Wilaya imekuwa ikipokea fedha za miradi ya maendeleo kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo ikiwemo miradi ya ujenzi wa madarasa, mabweni, maabara, mabwalo, nyumba za watumishi, zahanati, vituo vya afya, mabwawa na barabara. Fedha hizo ni kutoka katika vyanzo vya Mfuko wa maji (RWSSP), Mfuko wa barabara (Road Fund), TASAF, Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo kutoka Serikali Kuu (LGDG), Mfuko wa Pamoja wa Afya (HSBF), Mfuko wa EGPAF, Mfuko wa Jimbo (CDCF) na Mfuko wa UKIMWI.

Mafanikio yaliyopatikana ni kuongezeka kwa fedha za miradi ya maendeleo kutoka Tsh. 2,517,282,636.16 mwaka 2014/2015 hadi Tsh. 7,410,294,453 mwaka 2017/2018. Mchanganuo wa kila mwaka umeonyeshwa kwenye jedwali hapo chini

Jedwali 1; Mchanganuo wa fedha za miradi ya maendeleo.

Na.	Mwaka	Bajeti iliyotengwa	Kiasi cha Fedha kilichotumika katika Miradi ya maendeleo
1	2014/2015	3,470,711,000	2,517,282,636.16
2	2015/2016	2,063,529,000	5,185,708,082
3	2016/2017	7,445,000,193	5,299,840,286
4	2017/2018	8,151,003,460	7,410,294,453

Aidha Wilaya imepanga kutekeleza miradi 3 ya kimkakati katika mwaka 2019/2020, miradi hiyo ni Ujenzi wa soko la Kisasa Mto wa mbu, Ujenzi wa kiwanda cha kuchakata ngozi Makuyuni na Ujenzi wa mnada wa kisasa wa mifugo Losirwa. Miradi hii itasaidia kuongeza mapato ya halmshauri kwa kiasi cha Tsh. 680,000,000 kwa mwaka.

10.0 KITENGO CHA TASAF

TASAF awamu ya tatu ilizinduliwa katika Wilaya ya Monduli mwezi Julai 2014 kwa mpango wa kunusuru kaya Maskini lengo kuu ni kuwezesha kaya maskini kuongeza kipato, fursa na uwezo wa kugharamia mahitaji muhimu.Utekelezaji rasmi wa Miradi ya TASAF awamu ya tatu ulianza Julai 2015.

Miradi ya TASAF inalengwa kuwezesha walengwa kukidhi matakwa ya kupata mazingira rafiki ya kujifunzia na kujifunza, huduma bora na za karibu za Afya na Elimu, miradi ya ujenzi wa barabara ambayo inalenga kuwaongeza walengwa kipato kwa kulipwa ujira kwa kufanya kazi za mikono pamoja na miradi ya kiuchumi ya ufugaji wa mbuzi kienyeji na kuku wa kienyeji.

- Mwaka 2015/2016 Serikali ilitoa kiasi cha Tshs.1,619,119,916/=kwa walengwa wa kaya maskini 1,642
- Mwaka 2016/2017 Serikali ilitoa kiasi Tshs,1,430,627,770/=
- Mwaka 2017/ 2018 tulipokea Tshs 1,297,781,943/= kwa Walengwa wa kaya Maskini wapatao 5863 ambayo ni sawa na asilimia 182 ikilinganishwa na fedha iliyotolewa mwaka 2015. Hii iliwezesha wanufaika kutoka katika hatua ya umaskini sana na kuingia katika hatua ya juu kwa maana waliweza kuwapa mahitaji muhimu watoto wao ya Afya, Elimu na Lishe.

Miradi ya Miundombinu katika sekta za Elimu yenye gharama ya Shilingi 132,424,515.34 kwa mwaka 2015 ambapo :

- Ujenzi wa nyumba ya walimu wawili katika Kijiji cha Mbaashi kwa kiasi cha Tshs.74,330,469.13
- Ujenzi wa madarasa 2, Ofisi na vyoo vya matundu sita katika Kijiji cha Kiloriti Kipoku kwa Tshs.58,094,046.21

Kipindi cha 2016 hadi 2018 tulipokea kiasi Shilingi 294,747,796.63kwa ajili ya miradi ya miundombinu ifuatayo:

- Ujenzi wa nyumba ya waalimu (2 in 1) katika kijiji cha Moita Bwawani kwa Tshs. 73,565,317.57
- Ujenzi wa nyumba ya Mwalimu katika shule yaKiloriti Kipoku kwa tshs.73,235,110.59.
- Nyumba ya mtumishi wa Afya katika Kijiji cha Arkatan Tshs 73,706,094.77
- Ujenzi wa Zahanati katika Kijiji cha Kilimatinde kwa Tshs. 74,241,273.70. Hii ni asilimia 212 ikilinganishwa na miradi iliyotekelezwa kwa kipindi cha mwaka 2015.
- Ukarabati wa Barabara katika Kijiji cha Eluai kwa Tshs 73,642,800/=.
- Ukarabati wa skimu ya umwagiliaji Engaruka chini kwa Tshs 72,329,535/=.

Pia tulipokea kiasi Shilingi 502,680,446.98 kwa ajili ya ukarabati wa Mabwawa 5 ambayo ni:

- Ukarabati wa mabwawa ya Meserani chini Tshs 71,056,365/=
- Bwawa la Engarooji kwa Tshs 71,705,382
- Bwawa la,Lendikinya Tshs 71,109,611.51
- Bwawa la Mbuyuni kwa Tshs,71,109,611.51
- Bwawa la Meserani juu kwa Tshs.71,727,141.96

Miradi ya ujasiriamali wa walengwa 1,116 imetekelezwa kwa kununua mbuzi 1478 na kuku 2,923 yenye thamani ya Shilingi 222,855,800.45 Miradi hii ilitekelezwa katika Vijiji vifuatavyo:

- Ununuzi wa mbuzi katika vijiji vya:

- Lemoot kwa Tshs 24,776,785.71
- Jangwani kwa Tshs 24,795,219.64
- Nafco Tshs 24,776,787.71
- Oltukai kwa Tshs 24,818,096.25
- Mfereji kwa Tshs 23,852,113.27
- Mswakini juu Tshs. 26,589,312.65
- Lolkisale Tshs.26,589,312.64
- Emairete Tshs 23,852,113.27
- Mlimani ufugaji wa nyuki kwa Tshs.22,806,063.31

Kwa kipindi cha mwaka 2016 hadi 2018 tulipata ongezeko la miradi ya miundo mbinu, miradi ya ajira za Muda na Ujasiriamali ambayo haikuwepo kwa kipindi cha mwaka 2015.

11.0 Sekta ya Kilimo

Wilaya ya Monduli inayo mazingira mazuri ya kilimo katika baadhi ya maeneo. Eneo linalofaa kwa kilimo ni hekta 105,547.5 na eneo linalolimwa kwa sasa ni hekta 28,500. Kati ya hizo hekta 7,700 zinafaa kwa kilimo cha umwagilaji ambapo kwa sasa jumla ya hekta 3,200 zinamwagiliwa. Wastani wa mvua ni mm 500 ukanda wa chini hadi 1000 ukanda wa juu kwa mwaka. Mazao makuu yanayolimwa ni pamoja na mahindi, maharage, ngano, shayiri, mpunga na ndizi. Mazao yanayolimwa kwa kiasi kidogo ni kahawa, alizeti, choroko, kunde, ngwara, dengu , maua na tumbaku.Mwaka mzuri wa mvua wilaya ina uwezo wa kujitosheleza kwa chakula.

11.1 Usalama wa chakula wilayani.

Kufuatia msisitizo wa serikali na elimu juu ya umuhimu wa kaya kuzalisha chakula na kuhifadhi chakula cha kutosha ngazi ya kaya, hali ya usalama wa chakula imeongezeka wilayani. Uzalishaji wa mzao ya chakula umeongeeka toka tani 8,528 .4 mwaka 2015 hadi kufikia tani 13,698 mwaka 2018. Kipindi cha miezi ya Machi - Mei 2015 wilaya ilikuwa na upungufu wa chakula tani 2,004. Kipindi cha Machi - Mei 2018 wilaya haikuwa na tatizo la upungufu wa chakula. Bei ya mahindi imeendelea kuwa chini shilingi 25,000/= hadi 30,000 kwa gunia kwa muda mrefu kipindi cha 2018 tofauti na kipindi cha 2015 ambapo mahindi yalifikia hadi shilingi 90,000/= kwa gunia

11.2 Matumizi ya pembejeo:

Baada ya utaratibu wa Serikali wa kutoa ruzuku ya bei ya mbegu na mbolea za viwandani, mwamko wa wakulima kutumia mbegu bora na mbolea umeanza kuongezeka kwa asilimia 2.5 kila mwaka kuanzia 2015 hadi 2018. Mbolea inatumika zaidi na wakulima wa shayiri Monduli juu na mpunga Mto wa Mbu na Selela.

11.3 Ongezeko la uzalishaji kwa ekari

Elimu ya mbinu za kilimo chenye tija inayotolewa imewezesha ongezeko la uzalishaji wa mahindi toka gunia 5 kwa ekari 2015 hadi gunia 15 kwa ekari 2018. Hiki ni kilimo hifadhi ambacho wakulima hutumia kucha “ripper” mbolea za viwadani na viuua magugu.

11.4 Kilimo cha umwagiliaji

11.4.1. Miundo mbinu.

Mtandao wa kilimo cha umwagiliaji katika mabonde ya umwagiliaji ya Mto wa Mbu, Selela na Engaruka umeongezeka kutoka mita 13,500 mwaka 2015 hadi mita 14,300 mwaka 2018.Skimu zilizojengwa ni pamoja na Ormashine- Engaruka juu, Ormudana Engaruka juu, Endepesi Engaruka chini na Tindigani - Selela

11.4.2 Uhamasishaji wakulima wa umwagiliaji kuweka utaratibu wa uendeshaji na ukarabati wa skimu za umwagiliaji wao wenyewe.

Uhamasishaji ulifanyika umewezesha usajili wa skimu za umwagiliaji toka 0 2015 hadi 6 mwaka 2018.Skimu hizo ni pamoja na Engaruka juu, Engaruka chini, Kabambe Selela, Kabambe Majengo, Jangwani na Block Farm – Majengo.

11.5 Zao la mkakati

Wilaya imefanya sensa ya wakulima wote wa kahawa kwa lengo la kuinua uzalishaji wa kahawa wilayani. Kwa kuanzia jumla ya miche mipya ya kahawa yenye kuhimili magonjwa imeongezeka toka miche 450 mwaka 2015 had kufikia miche 3,500 mwaka 2018 Miche hi imepandwa katika shamba la Wilaya, shamba la shule ya “Maasae Girls” na wakulima wa vijijiji vya Mlimani na Olarash.

11.6 Program ya ASDP II

Baada ya program ya ASDP I kusimama mwaka 2015, wilaya imeanza utekelezaji wa Program ya ASDP II mwaka 2018 kwa kufanya mafunzo ya uhamasishaji, uelewa wa pamoja na Usimamizi shirikishi.

12.0 SEKTA YA USHIRIKA

Sekta ya ushirika kuanzia mwaka 2015 hadi 2018 imefanikiwa katika masuala mbalimbali kama ifuatavyo;

- ✓ Idadi ya Vyama vya Ushirika mwaka 2015 vilikuwa 33, kwa mwaka 2018 vimeongezeka hadi kufikia vyama 34
- ✓ Mitaji (hisa, akiba, amana) ilowekezwa na wanachama wa Vyama vya ushirika 2015 ni Tsh 637,937,000/= hadi kufikia mwaka 2018 uwekezaji umefikia Tsh.967,691,000/=
- ✓ Mikopo iliyotolewa mwaka 2015 ilikuwa Tshs. 1,687,560,000/= hadi kufikia mwaka 2018 mikopo iliyotolewa imefikia Tshs. **2,371,564,000** /=
- ✓ Bei ya kahawa kwa mwaka 2015 ilikuwa Tsh 4,238/= kwa kilo na kwa mwaka 2018 bei ya kahawa imepanda hadi kufikia Tshs 5,323 /= kwa kilo

13.0 SEKTA YA MIFUGO NA UVUVI

Ufugaji ni miongoni mwa shughuli muhimu za kiuchumi zinazofanyika ndani ya Wilaya ya Monduli. Zaidi ya asilimia 80 ya wakazi wa Wilaya Monduli wanajishugulisha na ufugaji. Wilaya ya Monduli ina jumla ya ng’ombe **284,687,** mbuzi **186,266** na kondoo **162,188**. Katika kipindi cha miaka 3 (2015-2018) kuna mafanikio makubwa katika nyanja za uthibiti wa magonjwa ya mifugo, uboreshaji wa mifugo ya Asili, kupiga chapa mifugo, uboreshaji wa mazao ya ngozi, usimamizi wa nyanda za malisho, kuongezeka kwa maduka ya Pembejeo za Mifugo na Dawa ya kuogesha Mifugo yenye Ruzuku 100%. Ujenzi na ukarabati wa

miundo mbinu ya mifugo (machinjio, majosho na minanda), uboreshaji wa sekta ya uvuvi na ongezeko la mapato yatokanayo na mifugo na uvuvi.

13.1 Uthibiti wa magonjwa ya mifugo

Kuendelea kutoa huduma za ugani kwa wafugaji ikiwemo utoaji wa chanjo za Mifugo ambapo uchanjaji mifugo umeongezeka kutoka ng'ombe **157,981** mwaka 2015 hadi ng'ombe **405,873** kwa mwaka 2018. Mbuzi kutoka 159,262 mwaka 2015 hadi mbuzi **368,423** mwaka 2018, Kondoo kutoka **142,614** hadi kondoo **239,579** mwaka 2018 na mbwa kutoka 1,429 mwaka 2015 hadi mbwa **3,674** mwaka 2018 waliochanjwa dhidi ya Homa CBPP, CCPP, Kimeta na kichaa cha mbwa na Mapele ya ngozi. Pia kuku kutoka 3493 hadi 9,347 wamechanjwa dhidi ya kideri, kuku kutoka 2331 hadi 8,163 wamechanjwa dhidi ya gumboro na kutoka kuku 2,631 hadi kuku 9,415 wamechanjwa dhidi ya ndui. Tumefanikiwa kuthibiti vifo vitokanavyo na magonjwa ya milipuko kama vile kimeta kutoka ng'ombe 26 mbuzi 34 na kondoo 37 mwaka 2015/2016 hadi mifugo 0 mwaka 2018 sawa na 100%.

13.2 Uboreshaji wa Mifugo ya Asili: Jumla ya ng'ombe majike wa maziwa kutoka 250 mwaka 2015 hadi 874 mwaka 2018 walipandishwa mbegu Kwa njia ya uhamilishaji na jumla ya madume bora wa nyama aina ya Sahiwal/Boran kutoka 14 mwaka 2015 hadi 57 mwaka 2018 na mabeberu bora kutoka 63 mwaka 2015 hadi 353 mwaka 2018 wa nyama aina ya Isiolo yamenunuliwa na taasisi pamoja na watu binafsi ndani ya Wilaya. Hii imepelekea kuongeza uzalishaji wa maziwa kutoka lita **10,530,000** hadi lita **13,500,000 mwaka 2018** kwa kipindi cha miaka 3.

Aidha kuku mitetea kutoka 1500 hadi 3500 na majogoo aina ya SASO kutoka 120 hadi 450 yamenunuliwa na kusambazwa kwenye vikundi vya wajasiriamali mbalimbali katika maeneo ya kata za Makuyuni na Mswakini pamoja na wajasiriamali binafisi.

13.3 Kupiga chapa mifugo

Aidha hadi kufikia mwishoni mwa mwaka 2018 Wilaya imefanikiwa kupiga kupiga chapa ng'ombe kutoka 0 hadi kufikia 1**88,940** sawa na asilimia **134.%** ya ng'ombe wote waliokuwa wamekusudiwa kupigwa chapa

13.4 Kuvuna Mifugo ya Asili na Unenepeshaji

Jumla ya mifugo kutoka 1,274 hadi 7,910 imenunuliwa na vikundi mbali mbali vya wajasiriamali wa biashara ya Mifugo kwa ajili ya kunenepeshwa na baadae kuuzwa mnadani kwa bei kati ya Tsh. 750,000 hadi 1,200,000. Aidha Wilaya kwa kushirikiana na mashirika yasio ya Serikali imewaunganisha wafugaji binafsi kutoka 0 mwaka 2015 hadi 17 mwaka 2018 na kutoka Vikundi 3 mwaka 2015 hadi Vikundi 72 mwaka 2018 vyenye jumla ya wanachama 360 na kupewa mkopo wa masharti nafuu wa jumla ya shilingi 588,500,000/=

13.5 Ongezeko la maduka ya Pembejeo za Mifugo: Maduka ya pembejeo za mifugo yameongezeka kutoka 13 mwaka 2015 hadi 27 mwaka 2018 katika maeneo ya Monduli Mjini, Meserani, Nanja, Makuyuni, Kigongoni, Mto wa Mbu, Selela na Engaruka.

13.6 Dawa za kuogesha Mifugo za Ruzuku

Wilaya imepokea dawa ya kuogesha Mifugo yenye Ruzuku 100% kutoka lita 0 mwaka 2015 hadi lita 118.75 mwaka 2018.

13.7 Kuongezeka kwa maduhuri yatokanayo na uvuvi.

Wilaya imefanikiwa kuongeza ukusanyaji wa maduhuri yatokanayo na mifugo kutoka Tshs.87,084,450/= mwaka 2016 hadi kufikia 155,885,658/=mwaka 2018 sawa na 79%.Hii ni kutokana na kuthibiti mianya ya utoroshaji mifugo minadani, lakini pia mifugo ya asili imeboreshwa kutoka 35% mwaka 2015 hadi 50% mwaka 2018 jambo ambalo limepelekea upatikanaji wa soko(bei nzuri) kwa mifugo hiyo na hivyo kuongezeka kwa maduhuri yatokanayo na mifugo.

13.8 Uboreshaji wa zao la Ngozi

Wilaya imefanikiwa kuongeza vikundi vya usindikaji wa zao la ngozi kutoka kikundi 1 mwaka 2015 hadi vikundi 5 mwaka 2018 vyenye jumla ya wanachama 150 katika maeneo ya Mto wa mbu, Mswakini na Makuyuni.Vikundi viwili vimefikia kiwango cha kuzalisha bidhaa zinazokaribia kufikia viwango vya ushindani katika soko. Hata hivyo kikundi kimoja cha Mto wa Mbu kimepata mkopo wa masharti nafuu wa Tsh. 4,000,000/= kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Monduli.

13.9 Ujenzi na ukarabati wa Miundombinu ya Mifugo.

Kwa kipindi cha Miaka 3 Wilaya imefanikiwa kuboresha miundo mbinu ya mifugo kwa kujenga na kufanya ukarabati kama ifuatavyo:-Mwaka 2015 kulikuwa na majosho 13 yaliyokuwa yanafanya kazi lakini hadi mwaka 2018 yameonengezeka hadi kufikia 19 , kati ya hayo 2 yamejengwa na 4 yamekarabatiwa.Ongezeko hili ni sawa na 46%. Mnamo mwaka 2015 hapakuwa na ukarabati wowote wa machinjio uliofanyika lakini hadi kufikia mwaka 2018 jumla ya machinjio 3 zimekarabatiwa katika maeneo ya Makuyuni, Baraka na Monduli mjini. Hata hivyo Wilaya imefanikiwa kufanya ukarabati wa Mitambo/Mashine ya kiwanda cha kuchakata nyama kilichopo katika machinjio ya kisasa Makuyuni. Mbali na hilo mnada 1 wa kisasa umejengwa katika kijiji cha Nanja na kufanya wilaya kuwa na minda ya kisasa 2.

13.10 Usimamizi wa nyanda za malisho, uchakataji na uhifadhi wa vyakula vya mifugo.

Wilaya imefanikiwa kuboresha usimamimizi wa nyanda za malisho kwa kuongeza idadi ya vijiji vilivyotenga maeneo ya malisho kutoka Vijiji 18 mwaka 2015 hadi Vijiji 23 mwaka 2018 sawa na ongezeko la 66% Vijiji hivyo pia vimefanikiwa kuunda kamati zamalisho ambazo zimepatiwa mafunzo ya namna ya usimamizi bora wa nyanda za malisho. Hata hivyo Wilaya imefanikiwa kuwa na kiwanda kidogo kimoja cha kuchakata vyakula vya mifugo kwa kutumia malighafi ya masalia ya mazao ya shambani kama vile mabua ya ngano na mahindi, magunzi, mashudu ya alizeti na kutengeneza marobota ya nyasi (bales).Ongezeko la kiwanda hiki ni sawa na 100% ukilinganisha na mwaka 2015 ambapo hapakuwa na kiwanda kabisa.

13.11 Uboreshaji wa sekta ya uvuvi

Wilaya imefanikiwa kuongeza vikundi vya wafugaji samaki kutoka 0 mwaka 2015 hadi 5 mwaka 2018 sawa na asilimia 100. Hata hivyo uchimbaji wa mabwawa ya samaki umeongezeka kutoka mabwawa 3 mwaka 2015 hadi mabwawa 11 mwaka 2018 sawa na 266% katika maeneo ya Mto wa Mbu, Majengo na

Migungani. Wilaya imehamasisha wavuvi wadogo wadogo wanaovua Ziwa manyara kufuata sheria, kanuni na miongozo inayoelekeza uvuvi salama. Hivyo kupunguza uvuvi haramu kutoka 50% mwaka 2015 hadi 35% mwaka 2018. Pia mwalo wa ziwa Manyara upande wa Monduli umekuwa chanzo cha mapato ya Halmashauri ambapo mapato yake yameongezeka kutoka Tsh.0 mwaka 2015 hadi Ths.10,477,000/= mwaka 2018.

14.0 SEKTA YA MAJI VIJIJINI

14.1 Hali ya Watumishi

2015; Wilaya ilikuwa na watumishi 13 (**Mhandisi 1** na **Wasaidizi 12**)

2018; Wilaya ina watumishi 23 (**Wahandisi 5** na **Wasaidizi 18**) sawa na ongezeko la watumishi 10

14.2 Upatikanaji wa Huduma za Maji Vijijini

2015; Idadi ya watu wanaliokuwa wanapata huduma ya maji **ni 89,040**

2018; Idadi ya watu wanaopata huduma ya maji ni **111,635** sawa na ongezeko la watu 22,595 ambapo ni sawa na 25.4%,

2015; hali ya upatikanaji wa maji ilikuwa **asilimia 52**

2018; hali ya upatikanaji wa maji imefikia **asilimia 74** kutokana na ujenzi wa miundombinu ya maji yenye jumla ya Tsh **4,342,179,689.00** katika Wilaya ya Monduli kama ifuatavyo:-

Ujenzi wa miundombinu ya miradi mipya ya maji

Na.	Jina la mradi	Kiasi kilichotolewa
1	Mradi wa usambazaji maji na usafi wa mazingira MONALI II	498,912,854
2	Mradi wa usambazaji maji na usafi wa mazingira kijiji cha Meserani Juu	444,867,916
3	Mradi wa usambazaji maji na usafi wa mazingira katika vijiji vya Emairete na Eluwai	609,271,552
4	Mradi wa usambazaji maji na usafi wa mazingira katika kijiji cha Lendikinya	605,606,643
5	Mradi wa ujenzi wa Bwawa katika kijiji cha Mbuyuni	740,094,820
6	Mradi wa usambazaji maji na usafi wa mazingira katika kijiji cha Nanja	1,077,000,000
	JUMLA	**3,975,753,785**

Ukarabati wa miundombinu ya miradi ya maji

Na.	Jina la mradi	Kiasi
1	Ukarabati wa chanzo cha maji kambi ya chui	31,729,459
2	Ukarabati wa mtandao wa mabomba katika kijiji cha Enguiki	25,000,000
3	Ukarabati wa mtandao wa mabomba katika kijiji cha Mfereji	55,250,000
4	Ujenzi wa tanki la maji katika kijiji cha Meserani juu	82,899,840
5	Ujenzi wa miundombinu ya maji katika Kitongoji cha Irerendeni kata ya Engaruka	82,546,605
6	Ukarabati wa Bwawa la Migwara	89,000,000
	JUMLA	**366,425,904**

14.3 Ulipaji wa madeni ya Makandarasi

2015; tulikua na Madeni ya Makandarasi wa miradi ya Maji Jumla ya **TShs. 2,682,340,709.80** ambapo hadi kufikia Mwaka 2018, Serikali imeshalipa Deni lote

14.4 Vituo vya Kuchotea Maji (DP)

2015; vituo vya kuchotea maji vilikua 462

2018; vituo vya kuchotea maji vipo 664 ongezeko la vituo 202

14.5 Matenki ya Uvunaji wa Maji ya Mvua

2015; Matenki ya maji yalikuwa 198

2018; Yapo matenki ya kuvuna maji ya mvua 219 sawa na ongezeko la Matenki 21

14.6 Vombo vya Watumiaji Maji (COWSOs)

kwa lengo la kusimamia na kuhakikisha uendelevu wa miradi ya maji iliyokamilika Halmashauri imeongeza uundaji na usajiri wa jumuiya za watumia maji kwa mujibu wa sheria ya maji Na. 12 ya 2009 kutoka **jumuiya 8 mwaka 2015** hadi kufikia **jumuiya 25 mwaka 2018** sawa na ongezeko la **Jumuiya 17.**

Wilaya imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kama vile TASAF, World vision, Mviwata, International institute for Environmental and Development - IIED na TPP kwa lengo la kuboresha huduma ya maji kwa wananchi wa Wilaya ya Monduli.

15.0 SEKTA YA MAJI MJINI

Mamlaka ya maji safi Monduli Mjiini (MOUWSSA) ilianzishwa mnamo mwaka 2005. Mamlaka hii ipo katika daraja C.

15.1 VYANZO VYA MAJI

Mamlaka ya maji safi Mjini Monduli inategemea vyanzo vya maji kama ifuatavyo;

- Maji mtiririko -2
- Visima virefu -2

VYANZO VYA MAJI	IDADI	UWEZO WA KUZALISHA MAJI.
i) Maji mtiririko Lolomsikio	1	I) Lita 18,476 lita kwa saa
ii) Maji mtiririko Beneth	1	II) Hakijapimwa (Hutegemea kipindi cha masika)
iii) Visima virefu	2	I) Kisima Namba.2 kilichopo Ngaramtoni ya juu, Arusha kinatoa lita 113,000 kwa saa II) Kisima Namba.3 kilichopo Ngaramtoni ya juu, Arusha kinatoa lita 128,000 kwa saa

15.2 MAFANIKIO

Kwa kipindi cha muda wa miaka 3, Mamlaka ya majisafi Mjini Monduli imeweza kuongeza idadi ya watu wanaopata huduma ya maji kutoka watumiaji 16,070 ya mwaka 2015 hadi kufikia watumiaji 21,201 hadi Disemba 2018. Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 32

15.2.1 JEDWALI LA TAKWIMU ZA MAFANIKIO LIMEONESHWA HAPO CHINI

IDARA	ENEO	MWAKA 2015	MWAKA 2016	MWAKA 2017	MWAKA 2018
MAMLAKA YA MAJI(maji mjini)	Ukusanyaji wa mapato ya ndani	292,093,234	283,836,034 (-2.8%)	376,026,227 (28.7%)	417,530,670 (42.9%)
	Mtandao wa mabomba ya maji	171.6km	175.00 km (2.0%)	179.65 km (4.7%)	180.5km (5.2%)
	Idadi ya wateja waliounganishiwa mita za maji	1,667	1,872 (12.3%)	2,027 (21.6%)	2,155 (29.3%)

IDARA	ENEO	MWAKA 2015	MWAKA 2016	MWAKA 2017	MWAKA 2018
	Idadi ya watu waliofikiwa na mtandao wa maji katika maeneo wanayoishi	16,070	18,440 (14.75%)	19,950 (24.14%)	21,201 (32.0%)

16.0 KITENGO CHA USAFI NA MAZINGIRA

Idara ya mazingira inasimamia usafi wa mazingira na uzoaji taka katika makazi ya watu mijini na vijijini. Aidha inasimamia tathmini ya mazingira katika uanzishwaji wa miradi kwa lengo la kulinda na kuhifadhi mazingira. Pia inashiriki katika shughuli za upandaji miti na kusimamia siku ya usafi kila jumamosi ya mwisho wa mwezi kwa kuhamasisha jamii kushiriki.

Mafanikio yaliyofikiwa katika kipindi cha 2015 hadi 2018 katika idara ya usafi na mazingira ni kama ifuatavyo;

- ✓ Halmashauri tayari imeandaa sheria ndogo ya kusimamia usafi na uhifadhi wa mazingira na kwa sasa iko Mkoani.
- ✓ Kuongezeka asilimia ya kaya zenye vyoo kutoka kaya kaya 19,560 sawa na 58% mwaka 2015 hadi 29,089 sawa na 86% mwaka 2018 kati ya kaya 33,819 zilizopo.
- ✓ Kuongezeka kwa idadi ya viwanda vidogo vilivyorasimishwa kutoka viwanda 6 mwaka 2015 hadi viwanda 16 mwaka 2018 ambapo idara ilivitembelea na kutoa ushauri wa usafi na uhifadhi wa mazingira.
- ✓ Kupungua milundikano ya taka zinazotupwa hadharani kutoka 4 hadi 0 kwa sasa angalau kila kata ina eneo la kutupa taka.
- ✓ Kuongezeka kwa mwamko wa jamii katika kufanya usafi na kuondoa taka katika maeneo yao kutokana na kampeni ya usafi aliyoianzisha mheshimiwa Rais wa jamhuri ya muungano wa Tanzania.

Jedwali linaloonyesha ongezeko la kaya zenye vyoo na kupungua Kaya zisizo na vyoo. 2015-2017

	MWAKA 2015	MWAKA 2016	MWAKA 2017	MWAKA 2018 (julai)
Zenye vyoo	19560=58%	20629=61%	24349=71%	29089=86%
Zisizo na vyoo	14259=42%	13190=395	9470=28%	4730=14%

17.0 KITENGO CHA TEHAMA

Katika kipindi cha miaka 3 sekta ya Teknolojia ya habari na mawasiliano imekua kwa kiwango kikubwa katika halmashauri ya Wilaya ya Monduli. Baadhi ya mafanikio ya sekta hii ni kama ifuatavyo;

17.1 Kupunguza gharama zisizo za lazima wakati wa kupanga mipango na bajeti na kuanzishwa kwa mfumo wa FFARS;

Serikali imeboresha mfumo wa mipango na bajeti (planrep) kwa kuufanya uwe wa kimtandao (*web based system),* mfumo wa mipango na bajeti umeboreshwa ili kwamba kazi hii iweze kufanyika kwa kutumia mfumo mmoja wa "computer" kawa nchi nzima na kwa kutumia intanet(web based). Hii imepunguza gharama zilizokuwa zinatumika katika kuzalisha vitabu na posho za kusafiri kwa ajili ya kwenda kuwasilisha bajeti kwani marekebisho yote yanafanyika kwa njia ya mtandao. Sambamba na hilo serikali imeanzina mfumo wa FFARS (Facility, Financial, Accounting and Reporting System) kwa ajili ya kusimamia fedha zinazotumwa moja kwa moja kwenye vituo vya kutolea huduma kama vile shule, zahanati na vituo vya afya.

17.2 Mifumo kuweza kuongea na kurahisha utoaji wa huduma;

Mifumo imewezeshwa ili iweze kubadilishana taarifa; kwa mfano taarifa zinazoingizwa kwenye mfumo wa planrep zinatumika katika mifumo ya matumizi yaani "Integrated finance information system" (IFMIS) Epicor na FFARS (Facility, Financial, Accounting and Reporting System),

17.3 Kuongeza ufanisi na kuondoa mianya ya upotevu wa mapato katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri,

Halmashauri kwa kutumia mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji mapato unaoitwa LGRCIS (Local Government Revenue Collection Information System) imeongeza ufanisi wa ukusanyaji mapato na kuacha kutumia vitabu katika ukusanyaji wa mapato. Pia LGRCIS imeunganishwa na mifumo mingine ya kifedha kama vile NMB, MPESA, TIGO PESA na Airtel Money, kwa kutumia GePG (Government electronic payment Gatway) katika kuunganisha mfumo huu na mfumo mkuu wa Epicor kwa ajili ya Matumizi ya fedha zilizokusanywa.

17.4 Ufanisi na kuondoa gharama katika ulipaji wa mishahara na kutoa hati ya malipo ya mishahara kwa watumishi

Kutumia mfumo wa GSPP (Government salary payment port) iliyounganishwa na HCMIS Lawson kwa ajili ya kulipia mishahara ya watumishi. GSPP imewezesha serikali kuacha kutoa vitabu vya hati za malipo ya mishahara (salary slips) badala yake watumishi wanaweza kupata hati zao kwa njia ya kielektroniki kwa kutumia mfumo huu. Hivyo GSPP imewezesha watumishi kupata mshahara na hundi za mishahara kwa wakati.

17.5 Kuboresha huduma za Afya na Elimu

Halmashuri imeongeza tija katika usimamizi wa huduma za afya kwa kutumia mfumo wa GOTHOMIS, mfumo ambao unatunza kumbukumba za wagonjwa na makusanyo ya Hospitali, vituo vya afya na zahanati. Pia mifumo ya BEMIS na PREM imesaidia katika kuongeza ufanisi wa usimamizi wa shule,

wanafunzi, walimu na rasilimali zote za idara ya elimu msingi na elimu sekondari kwa kupata Takwimu sahihi hivyo kuondolea Serikali gharama na kulea ufanisi.

17.6 Uwazi na uwajibikaji.

Halmashuri kwa kushirikiana na wizara ya OR-TAMISEMI Imefanikiwa kuanzisha tovuti ya halmashauri www.mondulidc.go.tz kupitia mfumo wa "government website framework system". Ambao umewezesha halmashauri kufahamika ndani na nje ya mipaka ya nchi. Pia Kupata matukio mbalimbali yanayofanyika katika Idara na sekta mbalimbali za Halmashauri.

18.0 KITENGO CHA BIASHARA

Sekta ya Biashara ina jukumu kubwa la kuhakikisha inawezesha kukuwa kwa uchumi shirikishi na Endelevu, Pamoja na kuweka mazingira wezeshi na endelevu kwa ajili ya ukuaji wa Viwanda na Biashara kwa Ujumla na kuwezesha ushiriki wa Sekta Binafsi, kuendeleza wajasiriamali katika kupanua uzalishaji pamoja na huduma.

Kumekuwa na Ongezeko la Wafanyabiashara ambao wanarasimisha biashara zao kwa kupatiwa leseni za biashara ambazo zinawawezesha kutambulika na taasisi za fedha ili kuwapatia mikopo na kuongeza mitaji yao ya biashara

MWAKA	IDADI YA WAFANYABIASHARA	ONGEZEKO LA WAFANYABIASHARA KWA MWAKA
2015	839	-
2015/2016	917	78
2016/2017	1012	95
2017/2018	1118	106

Wilaya katika kutekeleza sera ya Tanzania ya Viwanda mwaka 2015 ilikuwa na viwanda vidogo 55 hadi kufikia Desemba 2018 Wilaya imekuwa na Jumla ya Viwanda vidogo 129 hii ikiwa ni sawa na ongezeko la viwanda 74, Viwanda vya Kati mwaka 2015 vilikuwa 3 hadi Desemba 2018, Idadi imeongezeka na kuwa 7 ni ongezeko la Viwanda 4.

18.1 VIWANDA VIDOGO

NA.	AINA YA KAZI YA KIWANDA	IDADI MWAKA 2015	IDADI HADI DESEMBA 2018	ONGEZEKO
1.	MASHINE ZA KUSAGA NA KUKOBOA NAFAKA	15	37	22
2.	UTENGENEZAJI WA MATOFALI	9	17	8
3.	WACHOMEAJI WA VYUMA(WILDING)	11	31	20
4.	MAFUNDI SELEMALA	14	28	14
5.	MASHINE ZA KUSHONA ZENYE MASHINE	4	11	7
6.	UTENGENEZAJI WA MIKATE	0	2	2

NA.	AINA YA KAZI YA KIWANDA	IDADI MWAKA 2015	IDADI HADI DESEMBA 2018	ONGEZEKO
7.	MACHINE YA KUKOBOA KAHAWA	1	1	0
8.	UCHAKATAJI WA NGOZI NA KUSHONA VIATU	1	2	1
JUMLA		**55**	**129**	**74**

18.2 VIWANDA VYA KATI

NA.	AINA YA KAZI YA KIWANDA	IDADI MWAKA 2015	IDADI HADI DESEMBA 2018	ONGEZEKO
1.	MACHINJIO YA KISASA-MAKUYUNI	1	1	0
2.	UCHAKATAJI WA CHAKULA CHA MIFUGO -MAKUYUNI -MUNGERE	0	2	2
3.	UZALISHAJI WA KOKOTO NANJA ARKATAN	2	4	2
JUMLA		**3**	**7**	**4**

18.3 VIWANDA VIKUBWA

Wilaya pia imefanikiwa kupima na kutenga eneo lenye ukubwa wa Ekari 25,000 kwa ajili ya ujenzi wa Kiwanda Kikubwa cha Magadi Soda katika kata ya Engaruka hadi sasa Serikali imefanikiwa kuweka mipaka(demarcation) na kufanya tathmini kwa madhumuni ya kulipa fidia kwa wale wataoguswa na mradi Wilaya mwaka 2015 ilikuwa na tawi la benki moja ya NMB Monduli Mjini lakini hadi kufikia Desemba 2018 Wilaya ina matawi ya benki 5 ambazo zinatoa huduma katika Wilaya ya Monduli. Pia mwaka 2015 Wilaya ilikuwa na taasisi 2 ndogo za kifedha kwa ajili ya kutoa mikopo kwa Wajasiliamali wadogo wadogo, hadi kufikia Desemba 2018 Wilaya ina taasisi 4 ndogo za kifedha kwa ajili ya kutoa mikopo.

18.4 BENKI

Na.	JINA LA BENKI	MAHALI ILIPO	IDADI MWAKA 2015	IDADI HADI DESEMBA 2018	ONGEZEKO
1.	NMB	MONDULI/MTO WA MBU	1	2	1
2.	CRDB	MONDULI/MTO WA MBU	0	2	2
3.	BANKI YA POSTA TANZANIA(TPB)	MONDULI/MTO WA MBU	0	1	1
JUMLA			**1**	**5**	**4**

18.5 TAASISI NDOGO ZA KIFEDHA

Na.	JINA LA TAASISI	MAHALI ILIPO	IDADI MWAKA 2015	IDADI HADI DESEMBA 2018	ONGEZEKO
1.	WEDAC	MONDULI MJINI	1	1	0
2.	BRACK	MONDULI MJINI	1	1	0
3.	CAS	MONDULI MJINI	0	1	1
4.	FANIKIWA	MTO WA MBU	0	1	1
JUMLA			**2**	**4**	**2**

18.6 BIASHARA YA NISHATI YA MAFUTA (PETRO STATION)

Mwaka 2015 Wilaya ilikuwa na vituo vya Biashara za Nishati(Petro station) 6 tu kwa ajili ya huduma za mafuta ya Petroli,Diseli na Mafuta ya Taa, hadi kufikia Desemba 2018 Wilaya ina Vituo vya Mfuta 10 katika kata za Monduli mjini, Meserani, Makuyni, Migungani na Mto wa mbu.

Na.	JINA LA KITUO	MAHALI KILIPO	IDADI MWAKA 2015	IDADI HADI DESEMBA 2018	ONGEZEKO
1.	HAGG PETROLEUM	MONDULI MJINI	1	1	0
2.	KADO FILLING STATION	MONDULI MJINI	0	1	1
3.	HASS PETROSTATION	MESERANI	1	1	0
4.	TOTAL MAKUYUNI	MAKUYUNI	0	1	1
5.	KASTULI FILLING STATION MAKUYUNI	MAKUYUNI	1	1	0
6.	MTO WA MBU SERVICE STATION	MTO WA MBU	1	1	0
7.	PANONE CO.LTD	MTO WA MBU	1	1	0
8.	NJAKE PETRO STATION	MTO WA MBU	1	1	0
9.	SAKADA	MTO WA MBU	0	1	1
10	SANGO PETRO STATION LTD	MTO WA MBU	0	1	1
JUMLA			**6**	**10**	**4**

18.7 Urasimishaji wa Wafanyabiashara Wadogo Wadogo (Wamachinga) kwa Ugawaji wa Vitambulisho vya Vya Ujasiriamali.

Wilaya inaendelea na zoezi la ugawaji wa vitambulisho kwa wafanyabiashara wadogo wadogo, Wilaya imepatiwa Jumla ya Vitambulisho 4000 kwa ajili ya Wafanyabiashara wadogo wadogo. Zoezi la uzinduzi wa Ugawaji wa Vitambulisho lifanyika tarehe 27/12/2018 katika Kata ya Mto wa mbu na lilifanikiwa kwa asilimia kubwa.

19.0 SEKTA YA ARDHI NA MALIASILI

19.1 Sekta ya Ardhi:

NA.	MAFANIKIO HADI MWAKA 2015	MAFANIKIO MWAKA 2015 - 2018
1.	**Upimaji wa taasisi za umma:** Mwaka 2015 taasisi 10 za umma zilikuwa zimepimwa na kupatiwa hatimiliki.	**Upimaji wa taasisi za umma:** Taasisi za umma 60 zimeweza kupimwa na kuandaliwa hati miliki ndani ya kipindi cha miaka mitatu. Upimaji huu umesaidia kupunguza migogoro ya uvamizi wa maeneo ya umma.
2.	**Kodi ya Ardhi:** Makusanyo yatokanayo na kodi ya ardhi yalikuwa 139,234,263 kwa mwaka 2015	**Kodi ya Ardhi**: Makusanyo yatokanayo na kodi ya ardhi yameongezeka hadi kufikia 200,476,552.73 kwa kipindi cha miaka mitatu
3.	**Upimaji wa mipaka ya ardhi ya vijiji:** Mwaka 2015 vijiji vilivyokuwa vimepimwa ni 20.	**Upimaji wa mipaka ya ardhi ya vijiji:** Katika kipindi cha miaka mitatu Jumla ya Ardhi ya vijiji 16 imeweza kupimwa na kufanya Jumla ya vijiji vilivyopimwa kuwa 36.
4.	**Mipango ya Matumizi bora ya ardhi:** Mwaka 2015 vijiji vilivyokuwa na mipango ya matumizi bora ya ardhi ni 18 tu kati ya vijiji 62 vya wilaya ya Monduli sawa na asilimia 29%.	**Mipango ya Matumizi bora ya ardhi:** Vijiji 23 vimefanyiwa mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa miaka mitatu na kufanya jumla kuu kuwa vijiji 41 vyenye mipango ya matumizi bora ya ardhi sawa na asilimia 66.12% hivyo kumekuwa na ongezeko la zaidi ya asilimia 37.
5.	**Upimaji wa viwanja:**	**Upimaji wa viwanja:** Viwanja 300 vimeweza kupimwa kwa kipindi cha mwaka 2015 – 2018 sawa na asilimia 60 ya lengo lililokuwa limewekwa.
6.	**Utatuzi wa migogoro ya ardhi:** Migogoro mbalimbali ya ardhi imekuwa ikiripotiwa na kutatuliwa na hadi kufikia mwaka 2015 kulikuwa na migogoro 104 ya ardhi.	**Utatuzi wa migogoro ya ardhi:** Jumla ya Migogoro ya ardhi 59 sawa na asilimia 57 imeweza kutatuliwa kwa kipindi cha mwaka 2015 hadi 2018. Migogoro husika ni ya watu na watu, taasisi na hata migogoro ya mipaka ya vijiji na vijiji.
9.	**Ubatilishaji wa miliki za ardhi kwa mashamba pori:** Mwaka 2015 mashamba matatu ndiyo yalikuwa yamebatilishwa	**Ubatilishaji wa miliki za ardhi kwa mashamba pori:** -Mashamba pori 13 yamebatilishwa miliki zake kati ya mwaka 2015 na 2017 -Mashamba pori 8 yamebatilishwa miliki zake kati ya mwaka 2017 na 2018 Hii inasaidia kupunguza migogoro ya matumizi ya ardhi hasa ukizingatia

NA.	MAFANIKIO HADI MWAKA 2015	MAFANIKIO MWAKA 2015 - 2018
		ufinyu wa ardhi kwa sasa katika jamii za kifugaji.
10.	**Utoaji wa elimu ya Ardhi na Mipangomiji:** Kabla ya mwaka 2015 utoaji wa elimu ya ardhi na mipangomiji ulikuwa katika maeneo ya Monduli, Meserani, Makuyuni na Mto wa Mbu.	**Utoaji wa elimu ya Ardhi na Mipangomiji:** Kutanua wigo wa Utoaji wa elimu ya Ardhi na mipangomiji katika maeneo mbalimbali ambayo ni: Sinoni Ngarashi, Barabarani, Losirwa, Kisutu na Nanja, Engaruka. Elimu hiyo imesaidia wananchi kutambua umuhimu wa kupata hati miliki za maeneo yao na faida zake.
11.	**Mabaraza ya ardhi ya kata:** Mwaka 2015 kulikuwa na mabaraza ya ardhi sita tu ambayo ilkuwa ni sawa na asilimia 42.9.	**Mabaraza ya ardhi ya kata:** Ongezeko la mabaraza ya ardhi ya kata kutoka mabaraza ya ardhi 6 yaliyokuwepo hadi mabaraza 12 hivi sasa ambapo kwa sasa ni sawa na asilimia 85.7. Hivyo kuna ongezeko la asilimia 42.8 ndani ya miaka mitatu.

19.2 Sekta ya Utalii na Wanyamapori:

NA	MAFANIKIO HADI MWAKA 2015	MAFANIKIO MWAKA 2015 - 2018
1.	**Mapato yatokanayo na shughuli za utalii** Mwaka 2015 mapato yalikuwa Tsh. 72,000,000 sawa na asilimia 52.	**Mapato yatokanayo na shughuli za utalii:** Kipindi cha miaka mitatu Jumla ya shilingi 754,474,643.36 zimekusanywa kutokana na utalii wa picha na uwindaji wa kitalii. Makusanyo yamepanda kwa asilimia 60.
2.	**Uanzishaji na uhifadhi wa maeneo ya mambo kale,Miamba,Utamaduni, mila na desturi (GEOPARK):** Mwaka 2015 vivutio havikutambuliwa rasmi kwa kuwa aina hii ya hifadhi ya GEOPARK ni mpya.	**Uanzishaji na uhifadhi wa maeneo ya mambo kale,Miamba,Utamaduni, mila na desturi (GEOPARK):** -Jumla ya vivutio 4 vimetambuliwa rasmi katika kata za Selela na Engaruka juhudi za kuhifadhi maeneo haya kupitia GEOPARK chini ya mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) zinaendelea -Vikundi vinne vimeundwa vijiji vya Selela na Engaruka na kupatiwa mikopo kwa ajili biashara katika utalii huu mfano kuuza vitu vya kitamaduni kwa wageni.
3.	**Kuhamasisha na kuimarisha uanzishaji wa vikundi kwa ajili ya shughuli za Utalii wa kitamaduni:** Mwaka 2015 Jumla ya vikundi 4 vya utalii wa kitamaduni	**Kuhamasisha na kuimarisha uanzishaji wa vikundi kwa ajili ya shughuli za Utalii wa kitamaduni:** - Katika kipindi cha miaka mitatu jumla ya vikundi 10 vya utalii wa kitamaduni vimeanzishwa/kuhamasishwa katika kata 6 za Monduli Juu, Makuyuni, Mto wa

NA	MAFANIKIO HADI MWAKA 2015	MAFANIKIO MWAKA 2015 - 2018
	vimeanzishwa/kuhamasishwa katika kata 4 za Monduli Juu, Makuyuni, Mto wa Mbu na Esilalei	Mbu, Esilalei, Selela na Engaruka
4.	**Udhibiti wa migongano kati ya wanyamapori na binadamu:** Mwaka 2015 jumla ya vijiji 8 wananchi wake wapatiwa elimu juu ya kulinda mazao, mifugo na maisha yao kutokana na wanyamapori wakali na waharibifu,ambapo elimu iliyotolewa iliua;matumizi ya tochi zenye mwanga mkali,matumizi ya moto mashambani,ujenzi wa maboma hai na chili bomb.	**Udhibiti wa migongano kati ya wanyamapori na binadamu:** -Vijiji vilivyohamasishwa vimeongezeka kutoka vijiji 8 hadi kufikia 13 -Ujenzi wa maboma hai ya mfano 23 katika vijiji 13 kwa ajili ya kudhibiti mifugo kudhuriwa na wanyamapori mfano simba.vijiji vya Baraka, Lemoti, Losirwa, Nafco, Oltukai, Mswakini Juu, Mswakini, Esilalei, Naitolia, Nafco, Lolkisale, Lengolwa na Oldonyo
5.	**Kifuta jasho/kifuta machozi kutokana na wanyamapori wakali na waharibifu:** Mwaka 2015 jumla ya wananchi 229 walipatiwa kifuta jasho/macho Tsh.39,878,933.12	**Kifuta jasho/kifuta machozi kutokana na wanyamapori wakali na waharibifu:** Jumla ya wananchi 232 walipatiwa kifuta jasho/machozi Tsh.48,115,000
6	**Udhibiti wa ujangili:** Mwaka 2015 matukio ya ujangili yalikuwa 70.	**Udhibiti wa ujangili:** Mwaka 2018 matukio ya ujangili yamepungua kutoka asilimia 70 hadi kufikia 20 hii ni kutokana na kuanzisha mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na; -Kuunda mtandao wa kuzuia ujangili (Ant-poaching group) kwa kuhusisha wilaya ya Monduli, Manyara Ranch, RWMA, Tarangire National Park, Manyara National Park na Kikosi Dhidi Ujangili (KDU) -Kuanzishwa vituo 2 vya wanyamapori Engaruka na Selela kwa ajili ya kupambana na ujangili kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro
7	**Jumuiya ya hifadhi ya Wanyamapori (WMA):** Mwaka 2015 jumuiya moja (1) ya hifadhi ya jamii ijulikanayo Randilen WMA ilianzishwa kwa lengo la kuhusisha jamii katika uhifadhi na kunufaika na rasilimali hiyo.	**Jumuiya ya hifadhi ya Wanyamapori (WMA):** Maboresho ya uendesheshaji wa RWMA yamefanyika katika kipindi cha miaka mitatu ikiwa ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa ofisi, kuimarisha kituo cha doria na mageti 2 ya kuingilia wageni.

NA	MAFANIKIO HADI MWAKA 2015	MAFANIKIO MWAKA 2015 - 2018
	Mwaka 2015 Randilen WMA ilikua na jumla ya askari wa vijiji (VGS) 15 kwa ajili ya shughuli za doria dhidi ya ujangili na uharibifu wa mazingira	Idadi ya VGS imeongezeka kutoka 15 hadi kufikia 25,kwa ajili ya kuimarisha doria za kudhibiti ujangili na uharibifu wa mazingira
	Mwaka 2015 Jumuiya ya hifadhi ya Randilen (RWMA) imepata jumla ya Tshs 416,482,432.8 kutokana na shughuliza utalii wa picha	Mapato yameongezeka kutoka 416,482,432.8 hadi kufikia Tshs 614,910,679.00 katika kipindi cha miaka mitatu
	Mwaka 2015 uhamasishaji wa wananchi wa jumuiya juu ya jinsi yakutambua umuhimu wa uhifadhi na kufanya biashara ya utalii haukufanyika kwa vijiji wanachama	-Katika kipindi cha miaka mitatu uhamasishaji wa jinsi ya kutambua uhifadhi na kufanya biashara ya utalii ufanyika kwa vijiji 8 wanachama ambavyo; Lemooti, Nafco, Naitolia, Mswakini Juu, Lolkisale, Mswakini Chini,Oldonyo na Lengolwa.

19.3 Sekta ya Misitu

Na	MAFANIKIO HADI 2015	MAFANIKIO MWAKA 2015-2018
1	**Upandaji miti** : - Hadi kufikia mwaka 2015 miti 900,445 ilipandwa	**Upandaji miti**; - Miti 2,108,920 imepandwa katika maeneo mbalimbali ikiwemo mashule, majumbani,mashambani ,Zahanati, Msituni na maeneo ya wazi
2	**Matumizi ya majiko Banifu** -Hadi kufikia mwaka 2015 majiko 141 yalitengenezwa na kutumika katika vijiji sita. -Washiriki 300 walipatiwa mafunzo ya majiko hayo	**Matumizi ya majiko Banifu** -Mpaka sasa jumla ya majiko banifu na umeme wa nguvu za jua 3,278 yametengenezwa na yanatumika katika vijiji 13
3	**Ufugaji nyuki :** -Hadi mwaka 2015 kulikuwa na vikundi vinne(4) vyenye mizinga 80	**Ufugaji nyuki :-** **-** Mpaka sasa kuna jumla ya vikundi vya ufugaji nyuki 18 vyenye jumla ya Mizinga 965 ya kisasa pamoja vifaa vya kisasa.
4	**Uvunaji wa asali:-** -Hadi kumwaka 2015 ofisi ilikuwa haijawahi kuvuna Asali 0kgs	**Uvunaji wa asali:-** -Jumla ya kilogram 118 za asali zilivunwa na ofisi katika mizinga ya idara na jumla ya sh. 1,180,000/= zimekusanywa
5	**Utunzaji wa misitu:-** -Jumla ya kilometa 10 za mipaka zimehakikiwa na kuwekwa alama za kudumu (beacons) katika misitu ya hifadhi hapa wilayani	**Utunzaji wa misitu** -Jumla ya kilometa 111.62 za mipaka zimehakikiwa na kuwekwa alama za kudumu (beacons) katika misitu ya hifadhi hapa wilayani
	-Hadi mwaka 2015 msitu mmoja ulikuwa na Management plan 1	**-** Jumla ya misitu 3 ya hifadhi inazo management plan 3
	-Elimu ya uhifadhi endelevu wa misitu kwa watu 1000	-Elimu ya uhifadhi endelevu kwa watu 5000 ulifanyika
	Matukio ya Uchomaji moto Misitu:- **-**Hadi mwaka 2015 kulikuwa na matukio 3 ya uchomaji moto ovyo.	**Matukio ya Uchomaji moto Misitu:-** **-**Matukio ya uchomaji moto ovyo misitu yamepungua hadi 0 mwakaa2018

20.0 SEKTA YA BARABARA ZA VIJIJINI NA MIJINI - TARURA MONDULI

Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (Tanzania Rural and Urban Roads Agency – TARURA) umeanzishwa kwa Agizo la uanzishwaji wa Wakala la mwaka 2017 [The Executive Agencies (TARURA) Establishment Order, 2017].

20.1 Mtandao wa barabara

Wilaya ya Monduli ina mtandao wa Barabara wenye jumla ya Km 1019.46 ambapo Km 394 zinahudumiwa na Wakala wa Barabara Tanroads (lami km 132, changarawe km 262). Km 625.46 zinahudumiwa na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini - TARURA (Lami km 9.9, changarawe km138 & Udongo km 477.56) ambazo tayari zimeingizwa kwenye mfumo wa usimamizi wa barabara (DROMAS). Mtandao wa barabara unaosimamiwa na TARURA umeongezeka toka km 617 kwa mwaka 2015 na kufikia km 625.46 ongezeko la km 8.46 ambalo ni sawa na 1.4%.

20.2 Miundo mbinu ya barabara

Kwa kipindi cha miaka mitatu toka mwaka 2015 mpaka mwaka 2018 miundo mbinu ifuatayo imejengwa

- Madaraja 5 kati 10 sawa na ongezeko la 100% yamejengwa katika barabara za Selela – Mbaash (Daraja 1), Barabarani – Kilimani eneo la mtu wa Mbu (Daraja 1), Diwani road Mto wa Mbu (Daraja 1), Makuyuni – Lemooti (Daraja 1) na Kisongo – Moita eneo la Kipok Sekondari (Daraja 1). Madaraja hayo yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka.
- Vivuko vya maji (Drifts & pipe Culvets), Drifts 12 kati ya 42 sawa na ongezeko la 40% zimejengwa katika barabara za Kisongo - Moita (Drift 2), Moita – Kilimatinde – Ndukusi (Drift 3), Meserani Chini – Naalarami Drift 1), Monduli – Olarash – Kosovo (Drift 1), Emairete – Ilimorijo – Nanja (Drift 1), Lengolwa – Lemooti (Drift 1), Dodoma Jct – Lesimingori (Drift 1) na Monduli – Lendikinya – Mti mmoja (Drift 2). Pipes Culverts laini 83 kati laini 184 sawa na ongezeko la 45% zimejengwa katika barabara zilizofanyiwa matengenezo.
- Km 68 kati ya km 138 sawa na 49% za changarawe zimetengenezwa katika kipindi cha miaka mitatu.

20.3 Bajeti ya matengezo ya miundo mbinu ya barabara

Bajeti ya matengenezo ya barabara imekuwa ikiboreshwa mwaka hadi mwaka kwa ajili ya matengenezo ya mtandao wa barabara Wilayani Monduli unaosimamiwa na Wakala wa barabara za vijijini na Mijini - TARURA.

- Mwaka wa fedha 2015/2016 ziliidhinishwa jumla ya Sh.1,204,350,000
- Mwaka 2016/2017 ziliidhinishwa jumla ya Sh.938,460,000
- Mwaka 2017/2018 ziliidhinishwa jumla ya Sh.1,364,940,000 na
- Mwaka 2018/2019 zimeidhinishwa jumla Sh.1,290,080,000.

20.4 Mfumo wa usimamizi wa barabara (DROMAS)

Tunaipongeza Serikali yetu ya awamu ya tano kwa kuanzisha na kuanza kutumika kwa Mfumo wa usimamizi wa Barabara ujulikanao kwa jina Dromas (**District Roads Management System**) ambao unasaidia kutambua hali ya barabara, aina ya matengenezo yanayohitajika pamoja na kusimamia matumizi ya fedha za barabara.

20.5 Manufaa ya kuanzishwa kwa TARURA

- Kuchukua majukumu na shughuli zote za mitandao ya barabara za Vijijini na Mijini zilizokuwa zikifanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.
- Usimamizi wa karibu wa miradi kwa maana ya Wakala anashughulika na miradi ya barabara tu
- Kuwa Mamlaka kamili ya kiutendaji kwa maana ya kupanga, kusimamia na kutekeleza miradi ya Barabara

21.0 MAMLAKA YA VITAMBULISHO VYA TAIFA WILAYA YA MONDULI

Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (National Identification Authority -NIDA) Wilaya ya Monduli inajishughulisha na kazi za Usajili na Utambuzi wa watu (Raia wa Tanzania na wageni wakazi) katika Wilaya ya Monduli kwa lengo la kuwapatia Kitambulisho cha Taifa. Mafanikio yaliyoweza kufikiwa na Mamlaka ya Vitambulisho Monduli kwa kipindi cha mwaka 2015 hadi 2018 ni kama ifuatavyo;

21.1 Zoezi la Uandikishaji

Wilaya ilikadiria kuandikisha Wakazi 83,886 kutoka katika Kata Zote hadi kufikia 31.12.2018. Hata hivyo Ofisi ya NIDA Wilaya ya Monduli ilifanikiwa kuandikisha Wakazi 66,890 wa Kata zote Ishirini (20) zilizopo Wilayani Monduli sawa na 80% ya Wakazi 83,886 waliopaswa kusajiliwa.

Taarifa ya Usajili ni kama inavyosomeka kwenye Jedwali hapo chini:

Na	**Kata**	**Makadirio ya Idadi ya Wakazi**	**Idadi ya Wakazi Waliosajiliwa**	**Asilimia**
1	Monduli Mjini	4,756	3,924	82.5
2	Engutoto	4,263	3,536	83
3	Monduli Juu	4,902	4,006	82
4	Mfereji	2,698	2,499	93
5	Lashaine	2,794	1,915	68.5
6	Sepeko	7,441	4,961	67
7	Lepurko	3,953	2,839	69.2
8	Meserani	3,581	3,992	111.5
9	Naalarami	1,573	671	43
10	Moita	4,615	3,112	67.4
11	Lolkisale	3,254	2,564	79

Na	**Kata**	**Makadirio ya Idadi ya Wakazi**	**Idadi ya Wakazi Waliosajiliwa**	**Asilimia**
12	Lemooti	2,250	1,805	80.2
13	Mswakini	2,451	1,612	66
14	Makuyuni	5,651	3,955	70
15	Esilalei	8,882	7,725	87
16	Mto wa Mbu	5,471	3,855	70.5
17	Migungani	3,378	3,128	93
18	Majengo	4,054	3,665	90.4
19	Selela	3,065	2,955	96.4
20	Engaruka	4,854	4,171	86
JUMLA KUU		**83,886**	**66,890**	**80.0**

Chanzo: Ofisi ya NIDA Monduli, 2018

21.2 UPOKEAJI WA VITAMBULISHO

Jumla ya Vitambulisho **7,381** vimezalishwa na katika hivi vitambulisho vilivyo zalishwa tumepokea jumla ya Vitambulisho **5,797** kutoka makao kwa kata mbalimbali kama inavyo someka kwenye jedwali:

Na.	**KATA**	**VITAMBULISHO VILIVYOPOKELEWA**
1	Engaruka	266
2	Engutoto	1,034
3	Esilalei	64
4	Lashaine	30
5	Majengo	1
6	Makuyuni	4
7	Meserani	422
8	Mfereji	1
9	Migungani	2
10	Monduli Juu	31
11	Mto wa Mbu	1
12	Monduli Mjini	1,740
13	Sepeko	41
14	Watumishi	2,160
	Jumla	**5,797**

Chanzo: Ofisi ya NIDA Monduli, 2018

21.3 UGAWAJI WA VITAMBULISHO

Ofisi ya NIDA Wilaya ya Monduli imeendelea na zoezi la ugawaji wa vitambulisho na mpaka kufikia Mwezi Desemba tumefanikiwa kugawa jumla ya Vitambulisho kwa wakazi wapatao **5,022** na zoezi hilo linaendelea.

22.0 MAMLAKA YA MAPATO (TRA) MONDULI

Kuanzia mwaka 2015 hadi mwaka 2018, Mamlaka ya Mapato Tanzania imepata mafanikio katika Nyanja tatu;

1. Kuongezeka kwa makusanyo ya mapato.
2. Kuongezeka kwa matumizi wa mashine za kielektroniki.
3. Kukua kwa mapato sekta ya utalii.

22.1 Kuongezeka kwa makusanyo ya mapato

Makusanyo ya mapato ya Wilaya yameongezeka kutoka makusanyo ya Tshs.779,566,577.78 kwa mwaka 2014/2015 hadi Tshs2,325,828,115.61 kwa mwaka wa fedha 207/2018. Ongezeko hili ni sawa na ongezeko la asilimia 198. Makusanyo ya Mapato yamekuwa yakiongezeka kila mwaka, mwaka wa fedha 2015/2016 mapato yaliongezeka kwa asilimia 52%, mwaka wa fedha 2016/2017 yameongezeka kwa asilimia 37 na mwaka wa fedha 2017/2018 yameongezeka kwa asilimia 43.

22.2 Kuongezeka kwa matumizi ya Mashine za kielektroniki.

Ili kuongeza makusanyo ya mapato kwa hiari na kuondoa ukadiriaji wa mapato usio sawia, Mamlaka ya mapato Tanzania imeazimia kuachana na mfumo wa ukadiriaji wa makisio wa zamani na kuhimiza wafanyabiashara kununua na kutumia mashne za kielektroniki ili mwisho wa mwaka makadirio ya kodi yafanywe kutokana na mauzo ya mashine. Kutokana na juhudi zilizofanywa na serikali ya awamu ya tano watumiaji wa mashine katika wilaya ya monduli wameongezeka kutoka watumiaji 32 kwa mwaka 2015 hadi watumiaji 145 sawa ongezeko la asilimia 323.

22.3 Kuongezeka kwa mapato ya sekta ya utalii

Shughuli zitokanazo na Sekta ya utalii hasa mahoteli na mahema ya kitalii yameongezeka katika wilaya ya Monduli na mchango wake umeongeza makusanyo ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT) toka makusanyo ya Tshs.124,945,336/= kwa mwaka wa fedha 2014/2015 hadi makusanyo ya Tshs.495,068,160.40 kwa mwaka wa fedha 2017/2018 sawa na ongezeko la asilimia 296.

23.0 SHIRIKA LA UMEME (TANESCO) WILAYANI MONDULI

Shirika la ugavi umeme Tanzania (TANESCO) linajishughlisha na uzalishaji, usafirishaji na usambazaji umeme kwa wananchi wa Tanzania. Katika Wilaya ya Monduli, kuanzia mwaka 2015 hadi sasa limepiga hatua kubwa kuhakikisha kuwa karibu wilaya yote inapata nishati hii muhimu sana kwa maendeleo ya nchi. Hadi sasa wilaya imeunganishwa na nishati ya umeme kwa asilimia 53.

Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2015 hadi 2018 jumla ya vijiji 22, ambavyo ni Kilimatinde, Kipok, Moita, Kiloriti, Dukabovu, Lolksale, Nafco, Arkatan, Mti mmoja, Nanja, Mbuyuni, Mto wa Mbu, Kisutu, Kigongoni,

Esilalei, Selela, Engaruka chini, Engaruka Juu, Olarash, Monduli Mjini, Lendikinya na Sepeko vimeunganishwa na nishati ya umeme.

Mwaka 2015 jumla ya vijiji 24 vilikuwa vimepatiwa umeme ikiwa na jumla ya wateja 3,015. Kufikia mwaka 2018 jumla ya vijiji 33 vimepatiwa umeme ikiwa ni ongezeko la asilimia 53 ya vijiji vyote 62. Vilevile jumla ya wateja 6,100 wameunganishwa umeme hadi kufikia mwaka 2018 ikiwa ni ongezeko la asilimia 102.

Kwa upande wa taasisi zinazotoa huduma kwa jamii, jumla ya taasisi 117 zilikuwa zimeunganishiwa na nishati ya umeme kwa mwaka 2015 na hadi kufikia mwaka 2018 jumla ya taasisi 163 zimeunganishiwa na nishati ya umeme ikiwa ni ongezeko la asilimia 39.

Miradi yote yenye urefu wa jumla ya kilomita 254 yenye jumla ya transfoma 25 iliyofanyika na ile ambayo inaendelea kufanyika ikiwa na jumla ya kilomita 60 yenye jumla ya transfoma 14 inagharimu kiasi cha fedha za Kitanzania shilingi bilioni kumi na mbili milioni mia tatu sitini na tano na senti sifuri **(Tzs.12,365,000,000).**

Kwa ujumla, wilaya ya Monduli kwa sasa imeunganishwa na umeme kwa asilimia 53. Na mara baada ya kukamilisha miradi nane (8) inayoendelea asilimia itaongezeka na kufikia 66.

JEDWALI 1; Takwimu za Upatakanaji wa nishati ya umeme

MAELEZO	**2015**	**2016**	**2017**	**2018**	**Ongezeko**	**% kati ya 2015 na 2018**
Idadi ya vijiji vilivyo na umeme	24	28	28	33	9	53
Idadi ya wateja walio na umeme	3015	3615	4600	6100	3085	102
Idadi ya Taasisi zilizo na umeme	117	126	131	163	46	39
Idadi ya miradi iliyotekelezwa	116km	116km	0km	20.5km		
Idadi ya vijiji ambavyo vinapelekewa umeme chini ya mradi wa REA awamu ya tatu mzunguko wa kwanza kwa mwaka 2018/2019				8		

Naomba kuwasilisha

Iddi H. Kimanta
MKUU WA WILAYA
MONDULI